

KUDHANIA



Asanteni. Asante, Ndugu. Mungu akubariki, Ndugu.

Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, na kuinamisha kichwa chetu.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru asubuhi ya leo kwa majaliwa ya kuja tena katika nyumba ya Bwana, kukutana na watu hawa wapendwa, mchungaji huyu mzuri, mke wake, wapendwa wake. Tunaomba, Mungu, sasa tunapoketi chini kujifunza, kujifunza Neno, kwamba Wewe utakutana nasi, na kutupa Chakula kwa ajili ya nafsi zetu. Tunatamani jambo hili, Baba. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

³ Mnaweza kuketi. Tunahesabu haya kuwa ni majaliwa kurudi hapa tena asubuhi ya leo kwa ajili ya darasa hili. Kwa namna fulani nilikimbia huku chini bila kutarajiwa, kwa dakika chache tu, kuzungumza na Ndugu Littlefield na kufanya ushirika. Tulikuwa na wakati mzuri sana jana usiku hapa, tukiwaombea wagonjwa, na asubuhi ya leo, nami nikamwambia ningejaribu kurudi na kulihutubia darasa lake la shule ya Jumapili kabla hatujaondoka.

⁴ Kwa hiyo, muda ukiwa umeenda kidogo, nilikuwa na baadhi ya marafiki ambao ndio kwanza waje kuniona, nami nikazungumza nao *huko* nje. Halafu basi, nilipokuwa na nafasi, nilishuka kwenye orofa ya chini kuona jinsi kanisa hili li—lilivyojengwa kule chini, maana tunaajaribu kujenga moja nyumbani sisi wenyewe, nasi tunaipenda hii vizuri sana, sampuli hii, jinsi ilivyoundwa. Nakipenda hiki kirusha-sauti hapa, vyovyote mnavyokiita, kinaonekana kinaweza kushughulikia sauti vizuri sana.

⁵ Halafu tena, na—natumaini, kama hakuna mmoja wao aliye hapa, kama wapo, ni sawa, ninataka kuishukuru moteli hii hapa chini, Moteli ya City View, mahali nilipokaa jana usiku. Na ni mara chache sana maishani mwangu nilizowahi kukaa kwenye moteli bila malipo, lakini nilifanya hivyo jana usiku. Hata hawangenilipisha hiyo, sasa, hilo ni zuri sana. Mwanangu pia, huko kwenye—kwenye Moteli ya Lehi, hata hawakumlipisha hiyo.

⁶ Nami nasikia ya kwamba watu walioungana, wakija hapa mkutanoni, ama kitu fulani jana usiku, kwamba waliwapunguzia bei, na kadhalika. Kama mngali hapa, na mnaenda kuwaaga, washukuruni watu hao kweli.

⁷ Na wakati mwingine tungetaka, kuja hapa juu kwenye—kwenye mkutano mkubwa wakati fulani, mwajua, katika—katika mkutano. Natumaini hao watu watajaa kabisa

kila usiku tangu sasa na kuendelea. Mnajua, imeandikwa, “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa walio wadogo, mmenitendea Mimi.”

⁸ Na kwa ajili ya, kuzungumza na meneja asubuhi ya leo, zile sifa nzuri alizompa Ndugu Littlefield, ndugu yetu hapa. Akasema, “Vema . . .”

Nikasema, “Nataka kuwalipa.”

Akasema, “La, ime—imeshughulikiwa tayari.”

Nikasema, “Mnamaanisha Ndugu Littlefield alifanya hivyo?”

Akasema, “La, tunataka tu kukupa wewe.”

Nikasema, “Loo, jamani!” Nami nikasema, “Sitaki kufanya hivyo, bwana.”

⁹ Naye akasema, “Naam, naam.” Kasema, “Tunamheshimu sana Bw. Littlefield, jinsi anavyowashughulikia watu huku, maskini na kadhalika na kujaribu kumsaidia kila mtu.” Kasema, “Tunaheshimu hilo, kwa hiyo jambo dogo sana tunaloweza kufanya ni kuchangia tu sehemu yetu ndogo, namna hiyo, kumsaidia.” Hilo ni zuri kweli, nilijaribu kumfanya achukue pesa za moteli, naye asingefanya hivyo, kwa hiyo hilo ni zuri. Ninaomba tu ya kwamba Mungu atawabariki jamaa hao kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁰ Billy alisema mahali alipokaa kule Lehi, ya kwamba huyo alikuwa ni mmoja wa mama wazuri sana aliopata kukutana nao, aliyekuwa kule. Naye ilimbidi kukaa muda mrefu zaidi kidogo baada ya wakati wa kuaga, kasema, “Hiyo ni sawa, hakuna malipo ya ziada, hakuna. Hakitalipiwa hata kidogo.”

¹¹ Na—napenda kuishi na watu kama hao, ambao ni wazuri kweli. Na, mwajua, ukiwa na roho ya namna hiyo, unaweza kufanya kazi pamoja nao, wale walio na roho hiyo ambayo ni mbaya sana ndio ambao huwezi kufanya kazi nao, unajua, hao—hao ndio watu unaopaswa kuwachunga, ambao, huwezi kuwaambia chochote, ni wagumu kabisa sasa, hakuna haja ya kuzungumza, watafanya tu watakalo, na ni hivyo tu.

¹² Vema, kwa kawaida shule ya Jumapili huchukua saa nne au tano nyumbani, kwa hiyo, hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu tuna kama tu dakika arobaini na tano, hamsini hapa ambazo tungetaka kuzungumza kidogo tu, asubuhi ya leo, juu ya Neno.

¹³ Sasa, ninyi mlio na Biblia zenu, ninawatakeni mfungue pamoja nami, katika Biblia, kwenye Hesabu mlango wa 14, ninataka kusoma sehemu ya mlango wa 14 wa Hesabu, na hebu tuanzie kwenye yapata kifungu cha 37. Sasa, sikilizeni kwa makini somo hili:

Hata watu hao walioileta habari mbaya juu ya nchi, wakafa kwa tauni mbele ya BWANA.

Naye Yoshua—Yoshua, mwana wa Nuni, na Kalebu mwana wa Yefune, wakabaki hai miongoni mwa wale watu waliokwenda kuipeleleza nchi.

Kisha Musa akawaambia wana wa Israeli wote maneno haya: na hao watu wakaomboleza sana.

Wakainuka na mapema asubuhi, wakakwea juu ya mlima hata kileleni, wakisema, Tazameni, sisi tupo hapa, nasi tutakwea hata kwenda mahali Bwana alipotuahidi, kwani tumefanya dhambi.

Musa akawaambia, . . . (Sasa, sikilizeni jambo hili.) Musa akasema, Kwa nini ninyi sasa kuyahalifu maagizo ya BWANA? maana halitafanikiwa jambo hilo.

Msikwee, kwa kuwa BWANA hamo kati yenu; msipigwe. . . kuangamizwa mbele ya adui zenu.

Kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani wako huko mbele yenu, nanyi mtaanguka kwa upanga: kwa sababu mmerudi nyuma, msimwandame BWANA, kwa hiyo BWANA hatakuwa pamoja nanyi.

Lakimi wakathubutu kukwea mlimani, hata kileleni: ilaranduku la agano, na BWANA, . . . la BWANA, halikutoka humo maragoni, wala Musa hakutoka.

Ndipo Waamaleki, na Wakanaani waliokaa huko mlimani, wakatelemka, wakawapiga na kuwaangusha, hata wakafikilia Horma.

¹⁴ Sasa, hii ni shule ya Jumapili, kwa hiyo mna mwalimu mashuhuri hapa, Ndugu, Ndugu yetu wa thamani Littlefield, nami kwa namna fulani ninajisikia kusitasita kuhusu kulikaribia darasa la shule ya Jumapili, lakini ninapenda kupata msingi kidogo juu ya jambo hili.

¹⁵ Sote tunajua, sasa, ya kwamba haya. . . Yote yaliyotukia katika Agano la Kale yalikuwa ni mifano ya kile kinachoendelea sasa. Kama nilivyosema jana usiku, Mungu hutupa kivuli cha hasi kabla cha halisi hakijaja. Nalo Agano la Kale lilikuwa ni kivuli cha Agano Jipya, kama tu vile mwezi unavyoakisi kivuli cha jua mpaka jua lichomoze. Sasa, tunatembea katika kivuli cha mwezi usiku, lakini jua linapochomoza, basi tuna nuru halisi ya jua. Lakini mwezi huakisi tu nuru ya jua kutupa ile nuru tuliyo nayo.

¹⁶ Sasa, Agano la Kale lilikuwa ni mfano na kivuli cha Agano Jipya lijalo. Watu walitembea katika Nuru waliyokuwa nayo, wakati mwezi ukiakisi. Lakini sasa hiyo. . . Waebrania 1, “Mungu zamani za kale,” zamani za kale, “kwa njia nyingi,” namna nyingi, “alisema na baba zetu kwa manabii, bali katika siku hii ya mwisho alisema nasi kwa Mwanawe, Kristo Yesu.” Sasa, hilo ni tukufu.

17 Sasa, Israeli walikuwa wametenda dhambi, nao walikuwa wakinung'unika, wakilalamika, nao wakafika mahali palipoitwa Kadeshi-barnea. Na hapo kweli palikuwa ndipo kiti cha hukumu, kwa kuwa hukumu ilitoka hapo, na hapo ndipo Israeli walipohukumiwa, Kadesh-barnea.

18 Tunaambiwa ni mahali padogo jangwani, ng'ambo ya pili ya Yordani, ambapo—ambapo pana mitende michache. Nao... Mle ndani, kuna chemchemi moja kubwa ya maji, na chemchemi kadhaa ndogo, ambayo inamaanisha mfano mzuri tungeweza kuupata hapa wa Kiti cha Enzi cha Mungu kikiwa ni nyumba ya hukumu, na sehemu ndogo za hukumu zijazo, kwa sababu *Kadesh-barnea* maana yake ni “hukumu.”

19 Na hapo ndipo Israeli walipohukumiwa kwa sababu ya kuzozana kwao, na kutotii, na kukatizwa kwa mpango wa Mungu, mfano halisi wa siku hizi. Kanisa katika tofauti zake hukatiza mpango wa Mungu. Mungu anatutaka tukusanyike kama moyo mmoja, nafsi moja, nia moja, marudio halisi ya Pentekoste. Lakini mnaona, tunakuwa tofauti sana, na tunataka iwe *hivi*, nasi kamwe hatutaenda lisipoenda *hivi*, na *hili*, mbona... Loo, mnajua jinsi ilivyo. Tunaninii tu, sisi... Hilo ndilo... Mungu anatuleta kwenye kiti hicho cha hukumu tena, mnaona, kwamba hatuna budi kukomesha hilo.

20 Mungu ana mpango, na hebu tuingie moja kwa moja ndani yake na tuendeleo mbele. Usingoje na kujaribu kupata *hiki* na *kile*, jisogeze mwenyewe. Mungu atawasogeza wale aliowachagulia kwenda hivyo. Mnaona? Wewe chukua tu wako mwenyewe, ni msimamo wa—wako, chukua msimamo wako. Kama jamaa huyo mwingine hachukui, tunajuaje yeye... huenda hakupaswa kulipokea, “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Huh? “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Sasa, kama hivyo sivyo, basi Kristo alisema kitu cha uongo.

21 Sasa, nitafundisha juu ya somo la *Kudhania*. Ni *Kudhania* tu. Sasa, kama tulikuwa... Webster inasema *kudhania* ni “kuthubutu bila mamlaka halisi, ama kulichukua jambo kijuu juu.” Hiyo ndiyo maana ya neno *kudhania*, “kwenda bila mamlaka,” ama, “kulichukua tu kijuu juu.” Sasa, kuna watu wengi sana wanaofanya hivyo, kulichukulia tu kijuu juu. “Hilo ni sawa. Loo, ni sawa kufanya hivyo, hiyo ni kusema, kulichukua tu kijuu juu.” Sasa, huko ni kudhania.

22 Sasa, Israeli walifanya kosa baya sana walipofanya jambo hili, si Israeli tu, bali kila mtu hulifanya, litakuwa ni kosa baya sana unapodhania kutembea pamoja na Mungu, wakati Mungu hajakuita utembe pamoja Naye, ama unapodhania kuthubutu juu ya mambo ambayo si ya Kimaandiko, ukifikiri yatakuwa sawa; si sawa.

23 Hawa alidhania, alidhani ingekuwa ni sawa, kwa sababu Shetani aliwasilisha kitu kilichoonekana kizuri sana. Lakini

yeye alikidhania; hakikuwa ni Neno. Hutaki kufanya hivyo, unataka kudumu na Neno. Usiondoke kwenye Hilo, kaa papo hapo. Haidhuru kama unasimama... Pia, kumbukeni, watu ambao wamewahi kumfanyia Mungu lolote walisimama peke yao pamoja na Mungu. Barabarani kuna nafasi tu ya wawili, hao ni wewe na Mungu. Wewe...

²⁴ Watu waliowahi kufanya lolote chini ya kusadikishwa na Neno, walisimama peke yao: Martin Luther, John Wesley, na kadhalika, Finney, Sankey, Calvin, Knox, Spurgeon, wowote wale. Mnaona? Musa, Elisha, ninii... wote hao, walisimama peke yao juu ya Neno la Mungu. Na hivyo ndivyo inavyokupasa kufanya, ni jambo la kibinafsi. Huna budi kusimama juu ya Neno, kulichukua Neno la Mungu.

²⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Israeli walikuwa wamefikia mahali hapa ambapo Mungu, katika neema Yake na rehema, alikuwa amewasamehe dhambi za maasi yao yote. Baada ya mwujiza baada ya mwujiza, Mungu alisema, “Nimeonyesha ishara kuu kati yao,” katika vifungu vilivyotangulia, “Nimeonyesha ishara kuu, nao wamepuuza ishara hizi zote.” Walitembea tu moja kwa moja kupitia jambo hilo kwa vyovyote vile, na kufanya yale waliyotaka kufanya, yale waliyodhani wanapaswa kufanya, si yale Mungu aliyosema wafanye, yale waliyodhani wanapaswa kufanya.

²⁶ Sasa, hapo ndipo tofauti ilipo: Mahali tunapowazia inatupasa kufanya, huku Mungu akisema tufanye vinginevyo, hatuna budi kurudi na kulifanya kwa njia ya Mungu, la sivyo kamwe hatutapita mahali hapo. Jambo ndilo hilo. Huna budi kurudi moja kwa moja mahali ulipoachia.

²⁷ Niliambiwa si muda mrefu uliopita na kasisi fulani, alisema alialikwa ndani, kulikuwa na mtu aliyekuwa amepigwa kwa bombomu kifuani, namna *hii*, kapteni. Naye alikuwa amelala akifa, kwa hiyo ka—kasisi akaitwa kwake hemani, naye mtu huyo alikuwa akijitahidi sana, akijaribu kupumua. Nao walikuwa ndio kwanza wamtoe uwanjani. Na—naye akasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

Akasema, “Wakati mmoja ni—nilikuwa.”

Akasema, “Vema, afadhali uwe mara moja, unakufa.”

²⁸ Akasema, “Ninajua hilo.” Kwa sababu risasi za bombomu zilikuwa zimemkata mapafuni kwa njia fulani, aliniambia, kisha kasema kwamba—kwamba—a—a—alikuwa yuafa, mapafu yake yalikuwa yanajaa, anagugumiza kooni mwake.

Naye akasema, “Vema, sasa,” akasema, “wakati mmoja ulimjua Yeye?”

Kasema, “Naam.”

²⁹ Kasema, “Sasa, fikiria sana, popote ulipomwacha, papo hapo ndipo utakapompata, mahali ulipomwachia.” Hiyo ni

kweli. Jinsi hilo lilivyo kweli! Papo hapo ulipomwacha katika Neno, papo hapo ndipo itakubidi kurudi.

³⁰ Kama Mungu akisema...U—unaenda kanisani, hilo ni sawa, unalipa zaka zako, hilo ni sawa, unafanya mambo haya ya kanisa, hilo ni sawa, lakini basi, inaporejewa hapa kumpokea Roho Mtakatifu, ama kitu *fulani* katika Neno Lake, nawe unaondoka, useme, “Si—sijui kuhusu hilo,” papo hapo ulipomwacha, papo hapo, kamwe hutaenda mbali zaidi. Ukiwahi kumpata tena, utarudi moja kwa moja nyuma kule. Unaondoka kwenye barabara kuu, unaona, unachukua njia ya kando; ukirudi moja kwa moja kwenye barabara kuu tena, utamkuta Yeye akingojea papo hapo.

³¹ Sasa, hivyo ndivyo yule kasisi, yeye alisema, “Mtu huyu, nilimwambia, kasema, ‘Fikiria upesi!’”

Akasema, “Vema, siwezi kufikiria.”

Akasema, “Afadhali ufikirie!”

Basi angalieni, kasema, “Nuru ikaja usoni mwa huyo kapteni, kasema, ‘Ninaikumbuka.’”

Kasema, “Anzia papo hapo.”

³² Naye akasema, “Sasa, najilaza nipate kulala, naomba nafsi yangu Bwana ailinde.” Alimwacha wapi? Utotoni, kwenye goti la mama yake, na hapo ndipo alipompata tena. Mnaona? Itakubidi kurudi moja kwa moja, mahali ulipomwachia.

³³ Nao Israeli walikuwa wameanza, lakini walikuwa wameshindwa, nayo rehema ya Mungu, neema Yake, iliendelea tu kuwashikilia, na kuwashikilia. Ndipo basi akafika Kadeshibarnea, ndipo Musa akamchagua mtu mmoja kutoka katika kila kabila, na akawatuma watu kumi na wawili kwenda kuipeleleza nchi. Ndipo walipofika kule, loo, ni mchafuko wa jinsi gani uliokuwa miongoni mwao, loo, jamani!

³⁴ Hawa hapa wanarudi na kusema, “Mbona, kuna...Mbona, tusingeweza kuwateka! Mbona, Waamaleki, na Wakanaani, na Waperizi, na wa kila namna, miji yao mikubwa iliyozingirwa kwa kuta, na baadhi yao ni wakubwa sana, watu hawa, mpaka tunaonekana kama panzi kwao.” Loo, walivunjika moyo. “Sisi...”

³⁵ Sasa, huo si ni mfano tu wa kanisa siku hizi? “Ha—hatuwezi kabisa kufanya hivyo. Sisi...Mbona, nawaambia, ha—haiwezekani. Sasa, tumekuwa *hiki*, na hatuna budi kuwa kidogo *hivi*, na...” Mikutano ya mitaani iko wapi tena? [Ndugu mmoja anajibu, “La, si mingi sana, Ndugu.”—Mh.] Hiyo ni kweli, jamaa mdogo. Si—si mingi sana, tena. Iko wapi ile mikutano ya maombi ya usiku kucha tuliyokuwa nayo? Imekuwaje? Uko wapi ule uaminifu mkubwa na kukaza mwendo pamoja na Mungu? Kuna shida gani? Tumekatiliwa mbali kutoka kwake. Tuliweka tu, kidogo kidogo.

³⁶ Dhambi inavutia sana, sana. Loo, ni madoido, na ina m—mvuto mtamu sana, dhambi inao, haina hatia kabisa. Mbona, inaonekana ninii sana—inaonekana isiyo na hatia kabisa. Usiisikilize!

³⁷ Baada ya kitambo kidogo, Yoshua alipoiteka ile nchi Mungu alimwambia, “Angamiza kabisa kila kitu kilichoko huko, usiache chochote.” Mbona, ungeweza kuwazia baadhi ya hao wanawake wa Israeli wakimchukua mtoto mchanga? “Loo, si anapendeza? Angalia ninii yake. . . hata hana meno bado.”

Yoshua akasema, “Mwueni.”

Mama akasema, “Loo, mimi ni mama, siwezi kumwua mtoto huyo mchanga.”

“Lazima; mlete hapa.”

³⁸ Kwa nini? Huenda akaonekana anapendeza sasa, bali atakua na awe tu kama baba yake. Huwezi kuibembeleza dhambi. Haina budi kushikwa na, si kwa glavu, bali mikono mitupu. Tunataka kuwa wazuri, kila mtu anataka. Tunataka kuninii. . . Lakini *uzuri* ni nini? Tunataka kuwa wanyenyekevu. *Unyenyekevu* ni nini? Tunataka kujaa huruma. *Huruma* ni nini?

³⁹ Yesu, Mtu aliyejaa huruma, aliwapita watu elfu mbili ama tatu, watoto wenye vichwa vilivyojawa maji, viwete, vipofu, vilema, waliopooza, Yeye alikuwa na huruma, alifanya nini? Alienda mahali ambapo Baba alimwonyesha, mtu ambaye labda alikuwa na ugonjwa wa tezi kibofu ama kitu fulani, akamponya na kuondoka, na kuwaacha hao wengine, Mtu aliyejaa huruma.

⁴⁰ Sasa, watu siku hizi, maneno yetu ya Kiingereza huwapumbaza watu. Mnaona? Hiyo ni huruma ya kibinadamu, hiyo si huruma. Kuna tofauti kubwa sana kati ya *huruma* na *wema*. Hayo ni maneno mawili tofauti kabisa, nasi tunayatumia vile vile.

⁴¹ Sasa, Neno halitumii huruma zozote, halina budi kutiwa. Dumuni na hilo Neno, haidhuru linakata vibaya jinsi gani. Ungewaziaje lingewaangamiza watoto wachanga, wanawake wasio na hatia, na vitu kama hivyo, *wanavyojita*? Chachu moja ndogo huchachua donge zima.

⁴² Hilo ni jambo lile lile lililoanza huko nyuma pamoja na Hawa. Ilionekana ni ya kijanja sana, “Mbona, mtakuwa na hekima. Hakika hamtakufa, Yeye ni mzuri kupindukia, asingewaua. Lakini hakika hamtakufa.” Lakini Mungu alisema mtakufa. Hilo lilianzisha jambo hilo lote, papo hapo. Mnaona? Hamna budi kudumu na hilo Neno, haidhuru.

⁴³ Usidhanie; amini. Usitoe hoja, maarifa yana hoja; imani haina hoja, imani huishikilia tu. Vipi kama Ibrahimu angalitoa hoja? Wazia, vipi kama Ibrahimu angalitoa hoja? Umri wa miaka mia moja, aliishi na mke wake, ilikuwa ni dada yake wa kambo, tangu alipokuwa na umri wa kama miaka kumi

na saba, wakafunga ndoa. Mbona, maumbile yalionyesha ujana wake wote na uwanawake vikija pamoja, mume na mke, bila mtoto, alikuwa mgumba, naye mke alikuwa tasa, miaka arobaini baada ya kukoma hedhi, haiwezekani kabisa.

⁴⁴ Mbona, hoja zako zinge—zingeonyesha ya kwamba asingeweza kufanya hivyo, bali imani katika Neno ililishikilia. Mnaona? Imani haichukui hoja, imani hulishikilia Neno.

⁴⁵ Mtu fulani anasema, “Ni—ninaamini . . .” Nilikutana na wahudumu wengi, kasema, “Ndugu Branham, ninaamini hayo unayosema ni kweli, lakini kama ningefanya hivyo, unajua ningefanya nini? Ningekuwa nikiombaomba; wangenifukuza kanisani mwangu.” Ingewabidi tu kunifukuza. Mnaona? “Hakuna mtu mwingine angenikubali.” Yeye atakuchukua. Huwezi kuishi hapa milele, huna budi kwenda *Kule*. Unaona? Imani haijui hoja yoyote, inaamini tu, inakutenga na kila—kila kifungo, hakuna kitu, wewe dumu moja kwa moja na imani, hoja zitaondoka.

⁴⁶ Israeli walisema, “Sasa, hoja inaonyesha ya kwamba, vema, kama tukienda kule, mbona, hao, ninii, mmoja wa watu hao angeweza kuwapiga kumi wa kwetu. Wala sisi si taifa la kijeshi, sisi si watu wa kijeshi, tuna fimbo, na mikuki, na vitu ambavyo tumeokota, nyara. Hakuna mmoja wetu aliyefunzwa, tungefanya nini?” Hiyo ilikuwa ni hoja.

⁴⁷ Lakini Kalebu na Yoshua! Amina, haya basi, watu wa imani, watu waaminifu, watu waliojua Mungu alisema huko chini Misri, “Ninawapa hiyo nchi,” hilo linatosha.

⁴⁸ Wakapitia kwa hao watu. Hao watu walikuwa wakiomboleza, na kulia, wakisema, “Sasa, watoto wetu watakufa nyikani, wanawake wetu watabakwa, na sisi hapa, tutaangamia huku nje nyikani,” wakati Mungu alikuwa ameahidi angewapa hiyo nchi.

⁴⁹ Sasa, kumbukeni, Yeye aliwapa hiyo nchi, bali iliwabidi kupigania kila inchi yake, Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, hapo nimewapa ninyi.” Nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji.

⁵⁰ Sasa, ninyi watu mlioombewa, ninyi nyote jana usiku, mlikuwa hapa, mlio- . . .mtu fulani alikuwekea mikono, tukaomba, Uwepo wa Bwana ukashuka, akajifunua Mwenyewe moja kwa moja pamoja na Neno, kuonyesha jambo hilo, hiyo ilikuwa ni kweli kwamba Yeye yupo hapa. Hakuna kujipumbaza, hakuna kosa, upo, ni kweli, hatudhanii kitu kingine chochote. Tunaweka kando hoja, tunazitupa chini na kulichukua Neno. Lichukueni Neno, msonge mbele, Neno lilisema hivyo.

Sasa, unasema, “Basi ahadi ni yangu.”

⁵¹ Hakika, lakini utapigania kila inchi yake mpaka uwe sawa. Um-hum. Utachukua kila—utachukua kila hatua yake. Ni vita.

Ahadi ni yako. Hiyo ilikuwa ndiyo nchi ya ahadi, iliwabidi wapigane wapate kila hatua yake; nayo hiyo ahadi ni yako, lakini utapigania kila inchi yake.

⁵² Niliitwa kuninii, na Mungu, kuihubiri Injili miaka thelathini na mmoja iliyopita, nimepiga vita tangu wakati huo. Kila inchi ya ardhi nimeipigania, kwa Upanga wa Mungu, nikichukua ahadi, na kukatilia mbali.

⁵³ Mtu fulani aje, aseme, “Sasa, tutakuwa wa kundi la Kibaptisti.” Kasema, “Vema, huwezi kuamini *hilo*. *Hilo* halikuwa kwa ajili yetu.” Unafanya nini? Chukua Upanga, ukate na kujiweka huru nalo, na uendeleo kusonga mbele.

⁵⁴ Nilikuja pamoja na Wapentekoste, kasema, “Ukiambatana na kundi *hili*, hatutakuwa na uhusiano wowote nawe.”

⁵⁵ Hilo kundi lingine likasema, “Ukiambatana nao, hatutakuwa na uhusiano...” Kata ujifungue, endelea tu kusonga mbele. Naam. Endelea tu... Ilibidi kupigania kila inchi yake.

⁵⁶ Lakini ni kitu gani? Ni ahadi. Mungu alifanya ahadi, na tudumu nayo. Mungu aliliahidi. Haidhuru... Huna budi kuwa na vita. Kama kila kitu kikishuka, kivivu, mbona, wewe, una—unashinda nini? Wanashinda kwa Neno la Mungu na ushuhuda wao, Damu ya Kristo.

⁵⁷ Huna budi kushinda kitu fulani, na huna budi kuwa na vizuizi fulani. Nao watu wanaotofautiana, na kubishana nanyi, na kuwaambia ninyi ni watakatifu wanaojibingirisha, na kadhalika, wewe, yaliyowekwa mbele yako, ni jaribio. Kama hujapata hayo, basi hata huko vitani.

⁵⁸ Ni nini unajiunga na Kanisa...? Ulijiunga na Jeshi na kupata mafunzo kwa sababu gani? Ati kukaa kitako, kurandanda mitaani na kujionyesha? Hivyo ndivyo baadhi ya Wakristo wanavyotenda, kwamba tunataka kutegemewa. Hutategemewa, utadharauliwa, “Kwa maana wote wanaoishi kitauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.” Utwae Upanga, katilia mbali kila kitu ujiweke huru, na uzidi kusonga mbele.

⁵⁹ Yoshua, Kalebu, waliwatuliza watu.

⁶⁰ Wakasema, “Hatuwezi kuiteka, kamwe hatuwezi kuiteka, hivyo tu.” Mnaona, walikuwa wakiwaangalia Waamaleki, Yoshua na Kalebu walikuwa wakiangalia ile ahadi; hiyo ndiyo tofauti, inategemea kile unachoangalia.

⁶¹ Yoshua alisema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kufanya hivyo, tunaweza hata na zaidi. Mbona,” kasema, “hao ni mkate tu kwa ajili yetu.” Kwa nini? “Wanaonekana wakubwa, ni wakubwa, lakini tutakuwa na mkate mkubwa.” Kasema, “Mungu alitupa ahadi, na hofu yetu iko juu ya kila mmoja wao, bado wanatofautiana nasi, hata hivyo wanatuogopa.” Hakika. Kasema, “Hofu ya—hofu ya Bwana iko juu ya kila mmoja

wao, wanatuogopa kabisa.” Kasema, “Hima twendeni tukaiteke. Mungu alitupa hiyo, kwa hiyo ni yetu, hebu tusonge mbele na kuiteka.”

⁶² Loo, laiti ningeweza kulikusanya kundi hilo la Kipentekoste pamoja! Huyu Mfilisti asiyetahiriwa anayesimama huko nje, na kusema, “Hatuna budi kuwa na *haya* yote, na *haya* yote.” Upuuzi. “Itatubidi kwa namna fulani kuingia katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni tupate kuwa na ushirika pamoja nao.”

⁶³ Ushirika wetu unatoka kwa Mungu, si kutoka kwa baraza lolote la wanadamu na mafundisho ya sharti ya kujibunia. Sisi ni—sisi ni watu wa Mungu wanaotarajia ushirika kutoka kwa Mungu, hapo ndipo haki zetu zilipo, ziko pamoja na Mungu. Tunawezaje kushirikiana na Mungu isipokuwa tuwe na ushirika katika Neno Lake? Kwa sababu Neno ni Mungu, nalo Neno linafanyika mwili linapofanyika wewe.

⁶⁴ “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo.” Haya basi. Mnaona? Lakini Neno halina budi kudumu *hapa* ndani. Lisipokaa, mvua itanyesha, na, mbona, haliwezi kuzaa, kwa sababu huliadini. Haidhuru unakiri kuliadini jinsi gani, huna budi kuliadini.

⁶⁵ Vema. Kwa hiyo Israeli, Mungu alimwita Musa atoke, na kusema, “Nitaliangamiza taifa zima, kaa kando tu.” Musa akawaombea, akajitupa kwenye pengo, ilikuwa ni Kristo ndani ya Musa, mnaona. Mungu angeua ulimwengu wote wakati mmoja kwa sababu ya dhambi, lakini Kristo alijitupa Mwenyewe katika pengo kwa ajili ya jamii yote ya binadamu. Musa alijitupa mwenyewe katika pengo kwa ajili ya Israeli.

⁶⁶ Naye akasema, “Ulifanya ahadi, Mungu. Ulitoa ahadi ya kwamba utawapeleka kwenye ile nchi.” Hiyo ni kweli. Musa alimfanyia nini Mungu? Wakati ilipoonekana kana kwamba Mungu atafanya jambo fulani kinyume, alilitupa Neno njiani Mwake. Amina. Loo, ninapenda hilo! Sasa, ninajisikia kupaza sauti nikizungumza tu juu Yake, mnaona. Kuweka Neno njiani. Mungu hawezi kutembea juu ya Neno Lake Mwenyewe.

⁶⁷ Kasema, “Ulihidi kufanya hivyo. Ulisema ungewapeleka kwenye nchi nzuri iliyojaa maziwa na asali. Niliwaambia yale Wewe uliyosema, na sisi hapa, tuko mikononi Mwako.”

⁶⁸ Mungu alisema, “Nitalitwaa kundi hilo kaidi na kuwaacha waozee huko nyikani, lakini nitawachukua hao watoto wao ambao walisema kwamba hawataenda popote, wangeangamia nyikani, nami nitawavusha.” Hiyo ni kweli.

⁶⁹ Mnaona, dhambi ni mbaya sana. Dhambi ni nini? Ati kuvuta sigara? La. Kunywa pombe? La. Kusema uongo? La. Kufanya uzinzi? La, hiyo si dhambi. Hakuna dhambi kuhusu hilo hata kidogo. Mnaona? La. Kusema uongo si dhambi, kulaani, kutumia Jina la Mungu, hiyo si dhambi. Uh-uh. Kutokuamini ni dhambi. Naam. Sababu ya kufanya hivyo ni kwa sababu huamini. Jambo

ndilo hilo. Kwamba . . . Rudini kwenye chanzo chake. Mnaona? Mnaona?

⁷⁰ Unasema uongo, unaiba, unafanya uzinzi kwa sababu huamini. Hiyo ni kweli kabisa, “Lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Kabla hata hajaanza amehukumiwa, kwa sababu haamini. Naam. Sasa, unafanya hivyo kwa sababu wewe ni asiyeamini. Ukifanya hivyo, na kusema wewe ni mwaminio, wewe si mwaminio, ushuhuda wako mwenyewe, matunda yako yanathibitisha ya kwamba wewe si mwaminio. Unaona? Huna budi kuondoa hayo kabla hata hujawa mwaminio. Unaona? Sasa, dhambi ni kutokuamini, na, kutokuamini ni dhambi, hasa, na kwa hiyo, unaona, hiyo ndiyo shida.

⁷¹ Ndipo wakasema, “Vema, sasa, hebu niwaambie kitu, tumefanya mengi ya haya, kwa hiyo tutatubu tu. Tutapanda hapa juu, na kuomboleza siku chache, na kulia kidogo. Na—naye Mungu atatusamehe hilo, na tutaendelea moja kwa moja.”

⁷² Musa akasema, “Kwa nini mnazivunja amri za Mungu? Niliwaambia, kama nabii Wake, katika Jina la Bwana, ya kwamba mmekwisha.” Amina. Sasa, hiyo ni amri tu kama Yohana 3:16. “Mungu amemalizana nanyi, kwa nini mnajaribu kuinuka tena?”

⁷³ Kama vile, nilikuwa nikizungumza na jamaa fulani juu ya kunikosoa juu ya kuyashambulia madhehebu, Sina neno dhidi ya watu walio katika hayo madhehebu, ninaushambulia huo mfumo.

⁷⁴ Kama nilikuona ukielea mtoni hapa kuelekea kwenye maporomoko, nawe ulikuwa kwenye maskini mashua ndogo, nami nilijua ya kwamba mashua hiyo haitayastahimili maporomoko hayo, si ningekupigia makelele? Si kwamba sikupendi, ninakupenda, ni mashua hiyo itakayoanguka pamoja nawe. Naam, bwana.

⁷⁵ Ni kanuni hizo za imani na madhehebu ambayo yatavunjikia huko ng’ambo, kwa sababu ni kinyume na Neno. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ni kinyume, dumu na Neno. Usidhanie yako sawa, hayako sawa, ni kinyume na Neno la Mungu. Kwa hiyo dumu na Neno. Unaona? Sasa, na tunapona leo jinsi kanisa limefanya, matokeo yake yamekuwa nini?

⁷⁶ Jamaa huyu akaniambia, “Lakini, Ndugu Branham, umekosea.”

Nikasema, “Thibitisha nimekosea. Ni nani aliyekuwa mkuu kuliko John Wesley?”

“Unasema wewe ni mkuu kama John Wesley?”

⁷⁷ Nikasema, “Nisingeweza kuvaa viatu vyake. Lakini,” nikasema, “ninataka kukuuliza jambo fulani: Laiti hilo kanisa lingalika mahali ambapo John Wesley aliliacha! Lakini mlifanya nini? Mliweka kundi la akina Ricky na Elvis mle ndani,

nanyi mlfanya nini? Mlipotosha kitu kile kile alichohubiri na kutetea; Mungu amemalizana nanyi.”

Akasema, “Ninaandika tasnifu juu ya kanisa hili.”

⁷⁸ Nikasema, “Sijali unaandika tasnifu ngapi, Mungu amewakataa.” Nikasema, “Mungu alikataa kila shirika na kila dhehebu.” Aliwakataa Wapentekoste wenu. Wako wapi? Methodisti iko wapi? Baptisti iko wapi? Presbiteri iko wapi? Katoliki iko wapi? Lutheri iko wapi? Kila wanapofanya hivyo Mungu huwaweka kwenye rafu.

⁷⁹ Nami nitamwuliza mwanahistoria yeyote, nami nimetumia miaka kadhaa katika kuisoma historia, ninawatakeni mnionyeshe wakati wowote ambapo kanisa lolote liliwahi kuunda dhehebu, ambalo Mungu hakuliacha life papo hapo wala halikufufuka tena, ninawatakeni mnielekeze mahali hapo. Lilikufa papo hapo, kwa sababu lilimkataa Yeye kama Mtawala.

⁸⁰ Hivyo ndivyo Israeli walivyofanya hasa walipotaka kufanana na mataifa mengine. Walitaka mfalme, ndipo maskini Samweli, yule nabii, yule aliyejiliwa na Neno la Bwana, akasimama pale na kusema, “Nataka kuwaulizeni jambo fulani,” akawaita pamoja. Walitaka kufanana na mataifa mengine, yeye akasema, “Nataka kuwaulizeni jambo fulani: Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lililo kweli?” Haya basi.

Wakasema, “La, yote uliyosema yalitimia.” Loo, haya basi.

Akasema, “Je, nimewahi kuwasihi mnipe pesa kwa ajili ya riziki yangu?”

“La, Samweli, sidhani uliwahi kujichukulia sadaka.” Mnaona?

“Vema, basi Bwana anawatakeni mkae na kumruhusu Yeye awe Mfalme.”

“Loo, tunajua haya yote ni kweli. Unatwambia ukweli, lakini Samweli, tu—tunataka kuwa kama Wa—Wabaptisti.” Mnaona?

Kasema, “Endeleeni.” Na papo hapo wakapoteza ushirika wao. Papo hapo kanisa likapoteza ushirika wake.

⁸¹ Kama mkiandika kanuni zenu za imani, mipango yenu, mafundisho yenu, mafundisho yenu ya Biblia, kisha mumalizie kwa koma, “Tunaamini *haya*, pamoja na kadiri Mungu atakayotujalia kuwa nayo, atuonyeshe,” hiyo ni sawa, bali mkiandika kwa nukta, “Tunaamini *hili*, na hakuna kingine zaidi,” basi hilo linamfungia Mungu nje wakati mnapoweka nukta. Hiyo ni kweli. Kanisa linaninii, linaendelea kukua.

⁸² Kwa hiyo Huyo hapo. Mnaona? Kwa hiyo wasingeweza kwenda mbele zaidi, Israeli wasingeweza kwenda mbali zaidi, na kwa hiyo wakasema, “Vema, tutapanda juu tukatubu, kisha

tutajaribu tena. Tunajua ya kwamba Mungu ana moyo mwororo, kwa hiyo atatusamehe.”

⁸³ Naye anapanda juu, ndipo Musa akasema, “Makosa yenu: kuziasi amri za Mungu, Mungu amesema amemalizana nanyi, na hilo latosha. Afadhali mfanye vizuri mwezavyo, kaeni papa hapa, maana mtaoza papa hapa katika ninii yenu wenyewe—katika hali yenu wenyewe. Mlijiingiza katika jambo hili, mumejiweka hapa, kwa hiyo hapo mtakaa.”

⁸⁴ Sasa, hilo ndilo... *Hili* hapa, ndiyo kwanza nilisome, “Mlijiweka hapa, mmekufia hapa, mmekwisha kiroho, kwa hiyo hapa mtabaki. Hapo ndipo mtakapokaa.”

⁸⁵ “Vema, tutaenda kulijaribu kwa vyovyote vile.” Kwa hiyo akapanda juu na kusema, “Bwana, tusamehe, nakwambia, Bwana, haikutupasa kufanya hivi,” na kupaza sauti. Basi kesho yake wakasema, “Vema, ninyi jamaa wote, njoni sasa, hima twendeni.”

⁸⁶ Lakini wasingeweza kwenda pamoja na Neno, lile Sanduku, wala nabii hakuenda pamoja nao, alibaki mahali ambapo Mungu alimwambia abaki. Wakaenda wakisonga mbele na “milioni moja zaidi,” bali wakashindwa, hao Waamaleki na hao wengine wakawafukuza moja kwa moja nchini. Walitoka wakaenda wakidhanja wao... ya kwamba Mungu atakuwa pamoja nao.

⁸⁷ Sasa, nitaninii... Sina wakati mwingi sana. Tunakabiliwa na sikukuu, na sikukuu hiyo inaitwa Pasaka. Wamarekani hawa wanaojiita Wakristo...

⁸⁸ Natumaini sitatenda kama mjuaji, kama nikifanya hivyo, na—naomba mnisamehe, sivyo? Lakini ni vipi kamwe mimi... Kama ukipigilia msumari kwenye maskani ile, na kuuacha ulegee nusu, afadhali usiupigilie mle. Ya kwanza... Kama misumari hii yote ikipigiliwa namna hiyo, ninaogopa kusimama chini yake, huna budi kuipigilia ndani na kuishikiza, uweke presha kwenye nyundo.

⁸⁹ Nasi tunajenga Nyumba ya Bwana, pigilia msumari ndani kabisa, uushikize upande wa pili kwa thibitisho lake, na “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu,” uh-huh unaona, ukweli wa Mungu uliofunuliwa kiroho, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Loo, Hilo litasimama milele, maana misumari ya Injili ndiyo mnayopigilia.

⁹⁰ Mungu anaishikiza upande ule mwingine kwa kulithibitisha Neno, akilifanya lithibitisha yale liliyosema litafanya, amina, hilo... basi mumelipata. Neno linasema hivyo, naye Mungu anasimama papa hapa mbele zenu, na kuthibitisha ya kwamba ndivyo ilivyo. Basi mtaenda wapi kutoka hapo?

⁹¹ Sasa, angalieni, sasa, yote yatatukia kwenye asubuhi ya Pasaka, kutakuwako na maelfu na mamilioni ya dola yatakayotumiwa kwa maua ya Pasaka ya kuwekwa

madhabahuni, kama tu vile Kaini alivyofanya. Mnaona? Madhabahu haikufanyiwa maua, Kaini alilijaribu hilo, halikufanikiwa, madhabahu ilifanyiwa nafsi za wanadamu. Hakika.

⁹² Mungu hataki ua lako, anakutaka wewe madhabahuni. Unajaribu kufanya kibadala, wewe ndiye mtu wa hapo, mimi na wewe, sisi ndio wa madhabahuni. Lakini tunadhani hiyo ni sawa, “Mungu analikubali,” tunasema, na ni sawa, tunadhani ya kwamba hilo tu ndilo linalotubidi kufanya, ni kufanya hivyo tu.

⁹³ Sasa, tunaona ya kwamba maelfu yao hata hawatafanya hivyo, watatoka na kulewa. Wanajua ya kwamba wao ni... wanajua ni Pasaka, inawakilisha Pasaka, kwa hiyo wana shida nyingi, dhambi nyuma yao, kwa hiyo wanafikiri kama wakilewa, na kusahau yote, hivyo—hivyo ndivyo tu inavyowapasa kufanya. Hiyo ni Marekani, wanafikiri hivyo ndivyo tu inavyowapasa kufanya.

⁹⁴ Niliona tamasha la ajabu sana nililoona kwa muda mrefu, Ijumaa, nilipoenda kuwachukua watoto wangu shuleni, nilimwona mwanamke mmoja miongoni mwa kundi hilo, hakuwa anavuta sigara. Nikarudi na kumwambia mke wangu, nikasema, “Nimeona mwujiza.”

⁹⁵ Kila mmoja wa hao wanawake akitoka, “Halo, Liddy,” moja kwa moja kwenye vipandio, “ona mimi... *puu, puu, puu...*” Loo, jamani, wanaimba katika kwaya, ni wafuasi wa kanisa, wanadhani hilo ni sawa. Mtaona vinginevyo mwishoni mwa safari. Angalieni mahali mlipo sasa.

⁹⁶ Lakini wanawazia, “Vema, nawaambia tutakalofanya, tutaninii—tutaninii...” Baadhi yao wana moyo mwema vya kutosha kuchangia pesa za misaada, “Nilitekeleza wajibu wangu.” Hiyo si—hiyo si... hiyo si Pasaka, hiyo si Pasaka. Hilo ni jambo zuri, hamna neno dhidi yake, kuchangia misaada, hiyo ni sawa, lakini huo sio wajibu wako kwa Mungu, huo ni wajibu wako kwa mwanadamu mwenzako. Wajibu wako kwa Mungu ni kuyatoa maisha yako Kwake; pesa zako mpe mwanadamu mwenzako. Unaona? Mnaona jinsi tunavyolipata? Lakini wanadhani hilo ni sawa. “Loo, naam, hilo—hilo ni sawa.”

⁹⁷ Loo, baadhi yao wanauchukua ufufuo kwa mayai ya Pasaka, vitoto vya sungura. Vitoto vya sungura vina uhusiano gani na ufufuo? Mayai ya Pasaka na kofia mpya zina uhusiano gani na Pasaka?

⁹⁸ Mhubiri fulani aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, mimi,” ilikuwa ni mhubiri Mkampbeli, Mkristo, akasema, “Tlinibidi tu kuficha uso wangu na kucheka baadhi ya kofia za kuchekeka ambazo hao wanawake walikuwa wamevaa.”

⁹⁹ Nikasema, “Ulipeleka wapi somo lako?” Lipeleke mahali linapohitajika, usibembeleze-bembeleze na kuipapasapapasa.

Huwezi kuibembeleza dhambi, huna budi kuilaani. Hiyo ni kweli, laani hicho kitu, ni kosa, kiondokee.

¹⁰⁰ Bila shaka, kama alifanya hivyo, muda si muda mwajua, halmashauri ya mashemasi ingeyaandikia makao makuu, naye ingembidi kuondolewa moja kwa moja kwenye hilo dhehebu, lakini kwangu mimi, afadhali. . . na basi asingekuwa na kuku wa kukaangwa Jumapili. Loo, jamani! Mnaona? Mnaona? Asingevaa suti ya thamani kubwa mimbarani. Hakuna mtu mwingine ambaye angemtaka, dhehebu, kama akifukuzwa kutoka kwa moja, ametiwa alama mbaya pia kwa hao wengine. Mnaona? Kwa hiyo yuko kwenye ule ubao mkubwa kule juu.

¹⁰¹ Lakini nawaambieni, afadhali jina langu liwekwe kwenye kile Kitabu kikubwa *Kule* juu, kuliko ule ubao mkubwa *hapa* chini. Naam. Mnaona? Mungu atawapokea.

¹⁰² Lakini hawawezi kufanya hivyo, wanaliogopa. Wakidhani hilo ni sawa, kwamba Mungu ataelewa. Kweli anaelewa, anafahamu ya kwamba unapaswa kufanya yaliyo mema. Vema. Watu hunywa pombe, wanajaribu kuweka yaliyopita, na kuyasahau, kamwe hutayasahau.

¹⁰³ Wahubiri siku hizi wanahubiri mafundisho yao, tofauti zao, na kila kitu, wakidhani hilo ni sawa, makao makuu yalisema hivyo, hivyo ndivyo walivyofundishwa katika seminari. Wanafikiri hilo ni sawa, wakidhani tu ni sawa. Israeli walidhani pia, hawakufika popote. Mnaona? Usidhanie, hakikisha uko sahihi. Unaona? Sawa.

¹⁰⁴ Wanasema, “Vema, ni sawa, endelea, hiyo ni kusema, vema, mimi ni mfuasi wa kitu *fulani* hiki, nasi tunaamini hilo. Wazee we—wetu wa wilaya wanafundisha *hili*. Niniii ye—ye—ye—yetu,” (Mnaviitaje hivyo vitabu vidogo, wanavyoviandika, mwajua?), “kanuni zetu za imani na—na Mafundisho yetu yanaamini *hili*.”

¹⁰⁵ Kama ni kinyume na Neno, tupa kitu hicho kwenye kikapu cha takataka, na ulichukue Neno. Kuwa na sheria moja: upendo; Kitabu kimoja: Biblia; kuwa na kanuni moja ya imani: Kristo, na uendelee tu kusonga mbele. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Unaona?

¹⁰⁶ Ndipo hao watu, wanafanya nini? Wanakuja na kujiunga na mambo hayo. Natumaini sionekani katili kwenu, lakini sina budi kulifanya lishike. Inakubidi—inakubidi kushuka kwenda kule chini mahali fulani mpaka lishike kabisa. Uh-huh. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁷ Nilipoanza mazoezi ya ndondi kwa mara ya kwanza, kabla sijaingia katika mapigano ya kulipwa, kulikuwa na mkufunzi, kama walivyomwita, “Smith wa Sekunde Sita.” Pambano la kwanza la kulipwa alilokuwa nalo, alimshinda mtu huyo katika sekunde sita. Nami nilipoanza kufanyiwa mazoezi, mtu huyo nusura anieue, angenipiga anirushe moja kwa moja nje ya ulingo na kadhalika. Nami nilikuwa nikiruka kamba, na kukimbia maili saba, nane kila siku, na kuchukua mafunzo yote.

108 Nami nikasema, “Sita, kwa nini ikubidi kunifanyia hivyo?” Mnaona? Nikasema, “Umenitoa pumzi kabisa, jamani! Nilirushwa moja kwa moja juu ya kamba nne, nikatoka moja kwa moja mle kwenye. . .ka—katikati ya hivyo viti, na karibu nivunjike mgongo!”

Akacheka, akasema, “Hiyo itakufaidi.”

Nikasema, “Ati kunifaidi? Inawezaje kunifaidi? Nusura uniue!”

109 Naye akasema, “Angalia, Billy, sijali jinsi ulivyo mzima kimwili, mwili wako hauna budi kustahimili hilo, urudi upesi sana. Ukipigwa ngumi kali,” kasema, “kama mwili wako haujazoea kurudi, wewe utalala hapo na kuhesabiwa.” Akasema, “Lakini kama mwili wa—wako umezoea kupata hilo, kisha unarudi,” kila unapoupiga, hiyo huishtua damu, inairudisha moyoni, kasema, “ukifanya hivyo,” kasema, “basi mwili wako umezoea kurudi upesi. Ukibwagwa chini, unasimama tena.” [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Unaona? Kisha kasema, “Hilo halimaanishi kitu unapoangushwa chini, unasimama kwa miguu yako tena, upesi.” Kasema, “Unanichukia sasa, bali utanithamini utakapofika huko nje kwenye ulingo.” Hiyo ilikuwa ni kweli.

110 Ndugu, wakati mwingine inanibidi kumpiga konde mtu yeyote yule, lakini niligundua kitu fulani: Usiwabembezele, wamwagilie! Mtanithamini mtakapokuja Kalvari. Mnaona? Utakapofikia mwisho wa safari, utasema, “Mungu asifiwe, nina furaha nilipitia maskini njia hiyo iliyoparuza. Mimi huyu hapa nimesimama, nimeoshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo.” Mnaona? Msipige gumzo kwenye hizo kanuni za imani na kadhalika huko nje. Njoni, ingieni kwenye Njia. Mungu anayo Njia, mpango, uliandikwa papa *hapa* katika Biblia, hebu na tudumu nao.

111 Lakini watu wanakuja kujiunga na nini? Wanadhani wanafanya yaliyo mema, ndipo wanasema, “Mungu yuko wapi? Mungu wa Agano la Kale yuko wapi? Yuko wapi Mungu aliyewainua manabii? Yuko wapi Mungu aliyeahidi mambo haya yote?” Mbona, hakika Yeye hatafanya kazi kule, hawezi, hakuna kitu cha Yeye kufanyia kazi.

112 Maskini mama yangu wa kusini alikuwa akiniambia, “Unawezaje kupata damu kutoka kwa tanipu?” Haina damu ndani yake. Hiyo ni kweli. Utapataje ishara za kiroho na maajabu katika nyumba ya maiti iliyokufa, iliyoganda kikanisa?

Huna budi kupata Roho katika Mwili wa Kristo, hilo ni Neno Lake. “Maneno Yangu ni Roho,” alisema Yesu, Ndivyo yalivyo.

113 Sasa, watu wanajiunga, wanafikiri ni sawa, hiyo ni kweli, wakidhani ni sawa. Wahubiri wanaendelea kuhubiri fundisho la sharti la namna hiyo, huku wakijua Biblia inasema jambo lingine, watalihubiri kwa vyovyote vile, wakidhani wako

sahihi. Ni kitu gani? “Wakichukua mapokeo ya wanadamu na kuzitangua amri za Mungu.”

114 Wana—wana sehemu ya I—Injili, wanahubiri sehemu yake, hakika, wanachukua sehemu moja. Shetani alichukua karibu asilimia tisini na tisa ya Injili ambayo Mungu alimwambia Hawa, na kukubali ilikuwa ni kweli, lakini ilipofikia jambo hili dogo, yeye alisema, “Sasa, sisemi si kweli, lakini hakika, unajua ya kwamba hizo zilikuwa ni siku zilizopita. U—utakuwa *hivi*. Unaona?”

115 Usiongeze chochote, usiondoe chochote Kwake, lidumishe tu jinsi lilivyo, usidhanie chochote, amini tu Neno. Kama kanisa hilo la Kipentekoste lingalidumu na hilo, Unyakuo ungekuwa tayari umekwisha.

Loo, unasema, “Ngoja kidogo, Ndugu, sasa, sasa, ulisema jambo baya.”

116 La, sikusema, la, kamwe, najua nililosema. Mnaona? Katika siku za Nuhu. . . Biblia ilisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Katika siku za Nuhu, Mungu alikuwa mvumilivu, akaupitisha wakati kwa mbali, mnaona, hakutaka. . . hataki mtu yeyote apotee. Mnaona? Akaendelea mbele, zaidi, na zaidi, uvumilivu.

117 Ni jambo lile lile siku hizi, “kwa kuwa kama ilivyokuwa katika siku ile,” akingojea Kanisa Lake lipate kulitambua Neno Lake pamoja na Yeye, bali wanaendelea tu. Kila wakati Mungu anapomtuma mtu na kuhubiri kwa nguvu, mara tu anapondolewa jukwaani, kundi la akina Riki na Elvis wanakusanyika pamoja, mwajua, pamoja na D.D. zao kuu, wanaongeza *hili* Kwalo, na kuongeza *lile* Kwalo, na muda si muda mwajua yote yameondolewa.

118 Wapentekoste wetu vivyo hivyo, sehemu kubwa yao ikikana uponyaji wa Kiungu na kadhalika. Yale mabaya sana niliyopata kutendewa juu—juu ya uponyaji wa Kiungu yalikuwa ni wahudumu wa Kipentekoste. Mbona, ni—nilikodi ghala ya silaha katika mji *fulani*, nami sikuwa na viti vya kutosha kuwaketisha watu, nao watu maskini wakatoka kwenye vilima vya Arkansas kutoka kila mahali, wakija mkutanoni.

119 Nami nikaenda kwenye moja ya madhehebu makubwa sana ya—ya shirika la Kipentekoste, na ilikuwa, vema, kipimajoto cha kiroho kilikuwa tisini chini ya sufuri. Mbona, laiti ungaliliona! Naye mtu huyo alikuwa na yapata benchi mia tatu, walikuwa wamejenga kanisa zuri, kubwa. Hakika. Watu wanafikiri kwamba mafanikio ni ishara ya baraka za kiroho, hilo ni kinyume kabisa.

Basi nikamwuliza, nikasema, “Naweza kuchukua viti hivi? Nitakulipa *kiasi fulani* kwavyo.”

Akasema, “Nisingemruhusu mtu yeyote kukalia viti vyangu ambaye anaamini uponyaji wa Kiungu.” Hilo ni la Kipentekoste.

¹²⁰ Huko Kingston, Jamaika, kwenye uwanja wa mashindano ya mbio mwaka jana, ambako Bwana alikuwa akibariki, walikuwa na mhudumu wa Kipentekoste kule. Nami nilikuwa pamoja na Wafanyabiashara Wakristo, basi nikasema, “Tulikuwa na wafanyabiashara kutoka Kyuba, kutoka Haiti, na kutoka visiwa vya karibu, wameketi pale jana usiku. Nanyi jamani mlifanya nini . . . ?” Nikasema, “Ninawaonea aibu! Mlizingumzia nini? Msururu wa Magari ya kifahari.

¹²¹ “Nilikuwa jamaa mdogo katika biashara huko chini pembeni. Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Bwana alinipa *hiki*, Bwana alibariki *hiki*, na Bwana akakibariki *kile*.”

¹²² Nikasema, “Hao watu waliketi na kuangaliana.” Nikasema, “Nimekuwa pamoja nanyi muda mrefu vya kutosha, mpaka mnajua nilijua mioyo yao, Bwana alinijalia kuijua, niliona kile walichokuwa wakiwazia. Mnawaambia nini? Wao ni wafuasi wa nyumba hizi kubwa za maiti, nao wamefanikiwa, wao ni mabilionea.”

¹²³ Nikasema, “Jinsi mliyoy tofauti! Daima mkijivunia kile mlichyo nacho, na ni kiasi gani mlichokusanya katika muda *fulani-huu*.” Nikasema, “Ni tofauti jinsi gani na Pentekoste ya asili, waliuza kila kitu walichokuwa nacho na kuwapa maskini.” Nikasema, “Ninyi ni vinginevyo. Hao watu wanajua yote kuhusu maana ya kuwa tajiri. Wanataka kupata Kitu kinachoridhisha na kilicho na Uzima ndani Yake.”

¹²⁴ Usiku huo uwanjani, mahali nilipokuwa nikiwazungumzia, hao watu, baada ya kuwaleta kule, nilikuwa nikiwaambia habari zake, maskini jamaa mmoja akanijia na kusema, “Jinsi ulivyokosea!”

Nikasema, “Ati kukosea?”

¹²⁵ Kasema, “Naam, bwana. Wakati ulipotoa tamshi hilo kuhusu Wapentekoste kule nyuma, jinsi watu walivyoyuza yote waliyokuwa nayo,” kasema, “hilo ndilo jambo baya sana walilopata kufanya.”

Nikawaza, “Unaweza kuwa wa kilimwengu jinsi gani?” Mnaona?

Naye akasema, “Hilo lilikuwa ndilo ninii baya sana . . .”

¹²⁶ Nikasema, “Basi unataka kuniambia ya kwamba Roho Mtakatifu alifanya kosa? Kwani unamtumikia mungu wa aina gani kama yeye hufanya makosa? Yeye hana kikomo, ana nguvu zote, ni mjua yote.” Amina. Hakika. “Anawezaje kufanya kosa?”

Akasema, “Nitakuthibitishia walikuwa wamekosea. Huyu hakuwa ni Roho Mtakatifu.”

Nikasema, “Ati tendo la Roho Mtakatifu katika Biblia halikuwa ni Roho Mtakatifu?”

Akasema, “Angalia.”

Nikawaza, “Vema. U—ulijileta hapa nje, sasa, katilia mbali tu kiungo chako mwenyewe kwa msumeno.”

¹²⁷ Ni kama tu kumweka sungura zizini, kama unajua mahali kila sehemu ilipo, na kila shimo limezibwa, basi hana budi kurudia *hapa* apate kutoka nje, kaa tu papa *hapa*, itambidi kurudia hapa. Ataingiza kichwa chake katika kila shimo, bali kamwe hatatoka, mfungie tu, kaa papa *hapa*. Hivyo ndivyo ilivyo na mmoja wao, endelea tu kusonga mbele na Neno, weka tu Neno mbele yako, endelea kusonga mbele, umeziba kila shimo huko nje kwa vyovyote vile. Unaona? Endelea tu kusonga mbele, ukipanda juu.

Nikasema, “Basi ati Roho Mtakatifu alifanya kosa?”

Akasema, “Vema, hao watu walifanya kosa.”

Nikasema, “Walivuviwa na Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Angalia, Mhubiri, wakati mateso yalipokuja, na ubishi ukatokea miongoni mwao,” kasema, “huyo hakuwa ni Roho Mtakatifu.”

Nikasema, “La, bwana, lakini Roho Mtakatifu alikuwa katika ile huduma ya kwanza.”

Akasema, “Mateso yalipokuja, watu hao hata hawakuwa na makazi ya kuenda.”

¹²⁸ Nikasema, “Hivyo ndivyo Mungu alivyowataka wafanye, kwa hiyo walienda kila mahali wakilibiri Neno. Kama wanalikuwa na makazi, wanaliyarudia, lakini Mungu alikuwa akiusambaza Ujumbe. Wana Makao Mbinguni.”

Lakini hiyo ndiyo tofauti. Wanafanya nini? Wanadhania hilo ndilo jambo la kufanya. Silo jambo la kufanya, bila shaka silo.

¹²⁹ Sasa, wahudumu wanahubiri hilo, wakidhani ya kwamba itakuwa ni sawa; haitakuwa sawa. Wanaruhusu kusanyiko lao, wanawake wao kuvaa kaptura, kuvuta sigara, wanaume wao kufanya maskini karamu za kirafiki za karata, chumba cha kamari, michezo ya ulaghai kanisani, karamu za supu kumlipia mchungaji, kila kitu kingine ambacho ni cha kilimwengu. Watu wanajiunga, wakifikiri hilo ni sawa.

¹³⁰ Mbona, ninaishi karibu na parokia ya Kipresbiteri, na usiku wa manane hivi majuzi usiku kulikuwa na bugi-bugi nyingi sana zikiendelea kule kwenye orofa ya chini, mpaka ilikuwa—ilikuwa ni aibu. Ama, ni nini huku kujinyonganyonga kupya, wanakuitaje? Nanii wao...wao...hao wanawake wakivunja miguu yao na kadhalika, wakifanya hivyo? Mwajua, hiyo ni nini? *Mnenguu*. Wanahitaji mnenguu. Wanahitaji—wanahitaji fimbo ya Injili kuinyoisha itoke kwao, hiyo ndiyo wanayohitaji,

uamsho mzuri wa Injili ya kale, uliotumwa na Roho Mtakatifu. Wanahitaji kusokotwa, kweli, shingoni kwa kamba za Injili.

¹³¹ Lakini wanasema, “Loo, Yeye ni Mungu mwema.” Yeye *ni* Mungu mwema, lakini usidhanie hilo, Yeye ni Mungu wa haki pia. Yeye ni Mungu mwema. Kama vile maskini mvulana tineja alivyosema si muda mrefu uliopita, kasema, “Unajua, Mungu ni mwema sana Yeye kamwe hajali yale nifanyayo.” Upuuzi, Yeye anajali yale ufanyayo.

¹³² Naam, unasema, “Mungu ni Mungu mwema.” Mungu *ni* Mungu mwema, lakini tunasikia mengi sana ya hilo siku hizi. Mungu ni Mungu wa hasira, Yeye ni Mungu wa hukumu. Alikuwa mwema vya kutosha kushuka kule na kuwatoa Israeli moja kwa moja kutoka katika kinywa cha mauti, kisha akageuka moja kwa moja nyikani, na kuwaacha waoze kwa sababu wasingemfuata.

¹³³ Mungu alikuwa ni Mungu mwema kuwavuta ninyi Wapentekoste kutoka kwenye hayo madhehebu, bali mligeuka moja kwa moja na kutenda kama mama yenu, kwa hiyo mnaozea humo.

¹³⁴ Kuna kinasasauti kinachoendelea hapa, unaenda kote ulimwenguni, mwajua. Mimi zaidi sana sizungumzii *hapa* sasa.

¹³⁵ Lakini mnaozea moja kwa moja humo ndani. Ndipo basi naja kuwaambia ukweli, halafu hamuamini. Hili hapa limeandikwa papa *hapa*, mnaona, katika Neno. Naam, bwana.

¹³⁶ Loo, naam, wanadhania ya kwamba Yeye ni Mungu mwema, naam, bwana. Lakini Yeye ni...Hawaninii—hawadhaniai ya kwamba Yeye pia ni Mungu wa hukumu. Hapa ndipo Israeli ilipofanya kosa lake, walidhani Yeye alikuwa mwema sana, alikuwa amewafanyia mambo mengi sana. Hakika, Yeye aliwapandisha kutoka Misri, hakika alifanya hivyo. Alifanya miujiza, akachora mstari, akaweka ile Nguzo ya Moto kati yao na adui. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hakika, Mungu ni Mungu mwema, hakika. Akawajalia kuvuka Bahari ya Chumvi, na, uh, kuvuka Bahari ya Shamu, na kuvuka kwenda nyi—nyikani, na—na kadhaliika; Yeye ni Mungu mwema. Wakati, Wamisri walipoanza kuwafuatilia, mbona, Yeye aliwalinda katika saa ya kufa, akawaua Wamisri.

¹³⁷ Hakika, Yeye ni Mungu mwema, lakini subira Yake iliisha, ndipo wakati aliponena Neno hilo la mwisho, hilo lilitosha. Musa alisema, “Kwa nini mnazivunja sheria za Mungu? Mungu tayari amesema amemalizana nanyi.” Usidhanie mbali sana, Ndugu. Hiyo ni kweli. Huenda ukavuka mstari huo, hakuna kurudi. Unajua, kuna mstari. Mnawakumbuka wale waaminio wakwamia mpakani kule nyuma katika—katika Israeli? Wakwamia mipakani tu.

¹³⁸ Waebrania 6 inasema, “Haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na

kuvionja vipawa vya Mbinguni, kama watageuka, kujifanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri. Na kuihesabu ile Damu ya agano, waliyotakaswa nayo, kuwa ni kitu ovyo, na kuzifanyia jeuri kazi za neema.” Hiyo ni kweli. Mungu ni Mungu wa wivu; Yeye ni Mungu wa haki.

¹³⁹ Kama wewe ni baba na mama, nawe unawaambia watoto wako, “Mkienda *kule*, nitawacharaza.” Kama unampenda mtoto huyo, akivunja sheria zako, utatimiza neno lako. Hiyo ni kweli. Lakini ukimwachilia aendelee, “Vema, hilo ni sawa, lifanye tena.” Unaona? Hilo ndilo linalosababisha hawa wote hapa maskini akina Melinda, na akina Riki, na kadhalika hapa. Hilo ndilo linalosababisha uhalifu wa vijana.

¹⁴⁰ Baadhi yao huzungumza juu ya ujinga wa watu katika milima ya Tennessee na Kentucky. Ninawaambia, baadhi ya hao mama wazee huko nje wangewafundisha baadhi ya hawa Mayezebeli wa kisasa jinsi ya kuwalea watoto. Kweli. Acha mmoja wa watoto wao aingie na ninii yao. . . mwanamke. . . usiku. . . msichana huku nguo zake zote zimekunjamana mwilini mwake, amekuwa huko nje na Riki usiku kucha mahali fulani, akifanyiwa mapenzi kwenye gari, kisha aseme, “Ulikuwa na wakati mzuri, Kipenzi?” angechukua kijiti cha mhikori kutoka kwenye moja ya miti hiyo, wala asingetoka nje ya nyumba kwa mwaka mwingine. Bila shaka. Ati mnasema ni ujinga. Wanajua zaidi juu yake kuliko. . . Loo, afadhali ninyamaze hapo. Vema, tuendelee.

¹⁴¹ Sasa, Israeli walikuwa wakidhanja. Um-hum. Mnaona kile tunachoangua siku hizi, tukidhanja? Kiota kilichojaa mayai ya mwewe. Hiyo ni kweli kabisa. Wao si tai, hawajui lolote kuhusu mahali pa juu, jinsi ya kufika huko juu. Manyoya yao yamelegea sana wangebaki uchi wanapoanza kupanda hewani. Hiyo ni kweli. Mwinuko utayang’oa hayo manyoya, naye tai ndiye pekee aliye na manyoya ya kustahimili atakapofika huko juu. Manyoya yake yameotea ndani, yamefungiwa ndani, yakakazwa vilivyo. Amina. Anaweza kwenda juu sana hata koho, ama kunguru, ama mwewe wa kuku, angekufa akijaribu kumfuata.

¹⁴² Mungu alisema Yeye alikuwa Tai, “Mimi ni Yehova-Tai, na watoto Wangu wote ni tai wadogo.” Wanajua jinsi ya kuruka juu kule, ambako kuna ninii tu, huko juu ambako unasafirira. Amina. Loo, napenda kuwaangalia. Naam, bwana.

¹⁴³ Naam, akidhanja, alisema, “Loo, vema, Mungu hutusamehe mara nyingi sana, Yeye atatusamehe tena.” Kwa hiyo wakapanda juu.

Lakini Musa akasema, “Amemalizana nanyi. Mlipofanya hivi, mlivuka mpaka.”

¹⁴⁴ Hebu tuangalie nyuma tuone kama tulivuka mpaka au la. Yeye aliweka mpaka wapi kwa Walutheri? Yeye aliweka

mpaka wapi kwa Wamethodisti? Aliweka mpaka wapi kwa Wabaptisti, kwa Wakampbeli, kwa Wanazarayo, kwa Pilgrim Holiness, Kundi la Buddy Robinson, na wote hao? Yeye aliweka mpaka wapi? Mahali pale pale ambapo ameweka mpaka kwa Pentekoste. Waozee hapo! Mungu aturehemu. Hilo karibu linaniua, kusema hivyo, bali ninawajibika kwa Neno hili, kusema kweli. Lakini ni kweli, mtaozea papo hapo, halitainuka tena, hilo ni Neno la Bwana.

¹⁴⁵ Loo, mnadhania. Mwajua, Samsoni alidhania wakati mmoja pia. Samsoni alidhani ilikuwa ni sawa, Mungu alikuwa ni Mungu mwema, angeweza kuzurura na wanawake, angeweza kufanya lolote alilotaka kufanya, na ingekuwa sawa, angeweza kumfunulia siri za Mungu, na ingekuwa sawa. Mnaona ilikuwa ni kitu gani? Mwanamke, kanisa.

¹⁴⁶ Mwanamke anawakilisha kanisa katika Biblia. Delila alikuwa maskini Yezebeli yule wa siku hizo. Hiyo ni kweli...?...Kwa hiyo muda si muda mwajua, akajifunganisha kwake, naye mwanamke akamfunganisha kwa kidole, naye akafanya vile vile hasa...Ndipo akakuta kwamba nguvu zake zote zilikuwa zimemwishia.

¹⁴⁷ Hivyo ndivyo ilivyotendeka hasa kwa kanisa siku hizi, limejifunga kwenye kanuni hizi za imani, na mambo ya kujibunia, na mashirika, madhehebu, na kuliacha Neno la Mungu wakaingilia urasimu, kanisa linafanana na walimwengu wengine, na linatenda kama walimwengu wengine, na muda si muda mwajua, unakuta Roho Mtakatifu ameondoka. Nguvu za Injili ziko mbali nanyi. Kuna shida gani?

¹⁴⁸ Natumaini siwaudhi, bali natumaini nitawababua, ili kwamba mtaninii...Afadhali nibabuliwe kuliko kuchomwa moto, wakati wowote, kwa hiyo—kwa hiyo, sikilizeni, dumuni na Neno.

¹⁴⁹ Samsoni, alidhani ilikuwa ni sawa, Mungu alikuwa angali yuko. Hivyo ndivyo kanisa lilivyowazia, walipotoka hapa nje, “Vema, Mungu angali yuko. Yeye ni Mungu mwema, Yeye hajali.” Ninyi watu wa zamani hapa, wakati mama na baba yenu, huko nyuma, miaka hamsini ama sitini iliyopita, walipotoka kwenye hayo madhehebu, na kadhalika, wapate kuwa huru na Mungu, kumwabudu Mungu, na kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu, wakatoka Misri, mbona, kama ungalizungumza nao, kama wangerudi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile ambalo Wamisri walifanya, walimwengu, wangekucheka usoni mwako, lakini walifanya hivyo, walifanya hivyo, “Loo, tunadhani itakuwa ni sawa.” Usidhanie, dumu na Neno.

¹⁵⁰ Iliwabidi kupatana. Kwa nini ikawabidi kupatana? Mafundisho yenu makuu ya kiinjistili hata mkaingia ka—katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Mnafanya nini? Mnatenda kama tu wanavyotenda. Makanisa ni nini? Yanatenda

kama wanavyotenda. Shule zao ni nini? Jambo lile lile. Hata shule zetu za utakatifu zinazidi kuwa mbaya sana na mambo kama hayo, mpaka upotovu na kadhalika umekaa miongoni mwao.

¹⁵¹ Tunachohitaji ni nguvu za Mungu mle ndani kuikemea hiyo dhambi itoke, na papa hapa linabubujika, kasema, “Haya basi.” Hizo ndizo karama zinazotumwa Kanisani, bali wanafundisha theolojia nyingi sana, na sayansi, na—na kadhalika, mpaka wakamhuzunisha Roho Mtakatifu akaondoka. Hiyo ndiyo sababu wasichana wetu wanaokuwa mama mapema, na kadhalika, inatendeka, hiyo ndiyo sababu, dhambi ni nyingi sana miongoni mwetu, hiyo ndiyo sababu huwezi kuwaambia watu.

¹⁵² Wamesongwa sana na mambo ya ulimwengu, na shughuli za ulimwengu, na mambo ya... “Ili tu tupendwe na kanisa. Ili tupendwe na wazee wa jimbo. Kusudi tupendwe *hapa*.” Hiyo inaleta tofauti gani? Pendwa na Mungu. Acha wengine waende. Wakitaka kufuata, acha wafuate, wasipotaka, acha wakae mahali walipo, unaelekea kwenye nchi ya ahadi.

¹⁵³ Kama vile Mungu alivyomwambia Yoshua, mfano halisi wa hao wapa wanaotoka, Yeye alisema, “Mmekuwa kwenye mlima huu kwa miaka arobaini, mkizunguka-zunguka.” Walifanya nini huko nje miaka arobaini? Je, Mungu aliwalaani? La, aliwabariki. Loo, walioa wake, na kukuza mazao mazuri, na kuwalea watoto wachanga, na loo, wa—walikuwa na wakati mzuri sana. Mungu alikuwa pamoja nao, bali bado haikuwa ni ile ahadi.

¹⁵⁴ Sikilizeni, nitasema jambo fulani sasa, huenda likawababua, lakini sikilizeni: Hivyo ndivyo hasa Pentekoste imefanya, iliunda madhehebu kama ulimwengu, bali kamwe hawakuifikia ile ahadi kamili. Kweli walitoka Misri, walitoka, Mungu aliwashughulikia, akawaonyesha maajabu, na ishara, na miujiza, bali kamwe si kwa utimilifu wake. Mnajua ni kweli. Ndipo wale mashujaa wa kale wakafa. Hiyo ni kweli kabisa.

Sasa, hapo ndipo tulipofikia tena. Tumekuwa tukitangatanga kwa muda gani? Yapata miaka arobaini.

¹⁵⁵ “Mungu abarikiwe, mimi ni wa Umoja. Haleluya!” “Mungu abarikiwe, mimi ni wa Assembly.” “Utukufu kwa Mungu, mimi ni wa Church of God.” “Sisi ndio wa aina *hii*.” “Sisi ndio wa aina *ile*.” Ninyi si kitu; maadamu mnawazia hilo, si kitu ninyi.

¹⁵⁶ Biblia ilisema mtu anapojiwazia ni kitu fulani, yeye si ki- . . . yeye si—yeye si kitu anachopaswa kuwa. Hiyo ni kweli kabisa. Jione wewe si kitu. Shuka, kusudi Mungu aweze. . . Jifanye tupu, unajaribu kujijaza, jifanye tupu. Hiyo ndiyo kazi kubwa zaidi kwa Kanisa na kwa mtu binafsi, ni kujifanya mwenyewe tupu. Hilo ni kali, lakini ni zuri.

¹⁵⁷ Inanikumbusha tu wakati Mama, tulipokuwa watoto wadogo tulilelewa maskini sana, na kwa hiyo hatukuwa na

chakula kingi, naye Mama alikuwa akininii... Papa alikuwa akiokota ngozi za nyama kutoka kwenye tanuri mikate huko chini, wao, ambapo wangeoka hizo hemu na kadhalika. Na—nao wangeninii, Bibi Goodman, mwanamke mkongwe Mjerumani, yeye, wao walikuwa wakioka hemu. Walikata ngozi hizi kutoka kwenye hemu, naye Baba angeshuka kwenda kuzichukua, ndipo Mama angeziweka kwenye kikaango cha mikate.

¹⁵⁸ Loo, tayari wamesahau kikaango cha mikate muda mrefu uliopita, huko nchini mwangu, bila shaka, si ninyi wakusini. Nao wakaweka, pamoja na maskini hizo ngozi za nyama mle ndani, na kuzirudisha jikoni na kuzioka, mwajua, namna hiyo, na kutoa grisi yake ikatumike kwenye ugali wa mahindi. Nasi tulipika ugali wa mahindi kwa ajili ya kiamshakinywa, tulikuwa na molasi ya mtama na ugali wa mahindi, na hizo ndizo tulizokula. Wakati wa chakula cha kutwa, tulikuwa na mboga za majani, kama zilikuwako bado, mbaazi macho meusi, ama kitu kama hicho. Nasi tulikuwa na chakula duni sana na kadhalika.

¹⁵⁹ Mama, kila Jumamosi usiku, shuleni, angetuogesha sote, wote katika beseni ile ile, maji yale yale, anaongezea tu kidogo zaidi, mwajua. Unaposhuka kutoka kwenye... kwenye... unamsafisha yule mdogo kwanza, basi wa mwisho alipata uchafu wa hao wote, lakini tulifanikiwa, tukafaulu.

¹⁶⁰ Usafi sio sana sana ati uoshe nje, lakini vipi kuhusu ndani? Kuta zilizopakwa chokaa, kung'arisha makaburi nje, lakini ndani, mifupa ya wafu. Mko karibu sana leo, matangazo yote ya televisheni na kadhalika, kwamba mwondoe uchafu mikononi mwenu, kwa sabuni nzuri, na hayo yote ni uongo.

¹⁶¹ Nilikuja nyumbani hivi majuzi na kuona kitu fulani kwenye—kwenye televisheni, ama matangazo ya televisheni, ama *chochote kile*, nikisimama chini kwenye kituo cha petroli, mtu huyu akasema, “Loo, hata haikubidi kuosha vyombo tena, vitumbukize tu mle ndani na kila kitu kitaondolewa mara moja. Viweke tu.”

¹⁶² Nikasema, “Nitakuoshea vyombo, Meda.” Nilitaka... Nikaenda nikachukua chupa ya kitu hiki, nami nikasema, “Nitaosha vyombo.” Basi nikakitupa mle ndani, mapovu yakainuka *hivi*, ndipo nikatia hivyo vyombo ndani, na kuviacha vikae nusu saa kisha nikavitoe, mayai yalikuwa yangali juu yake. Upuuzi! Hivyo ndivyo wanayopata haya yote... Unaposikia tangazo hili lote kubwa, wakati kitu chochote kinapotangazwa sana, hakuna chochote kwake. Kama bidhaa ni nzuri itajiuzwa yenyewe.

¹⁶³ Hivyo ndivyo ilivyo kwa dini ya kale, si lazima uonyeshe mambo makubwa mno, na madhehebu makubwa, itajiuzwa yenyewe, kama ina nguvu za Mungu ndani yake. Ina *viondoa-dhambi* vingi, mnavyoviita, “Jiunge na *hili*,” na “Sisi ni *hili* takatifu, na *lile* takatifu,” ni utakatifu wa bure. Hiyo ni kweli.

Mungu Ndiye pekee anayeweza kuondoa dhambi, Damu ya Yesu Kristo, Naye hufanya hivyo unapoanguka katika karai Yake ya kuoshea. Hiyo ni kweli. Yeye Ndiye pekee anayeweza kufanya hivyo.

¹⁶⁴ Samsoni alidhani ya kwamba kila kitu kilikuwa sawa hata hivyo, Mungu alikuwa ndio kwanza amemfanyia mambo mengi sana. Hivyo ndivyo tulivyowazia, Mungu alifanya mambo mengi sana. Israeli waliwazia jambo lile lile, “Vema, Mungu amefanya hivyo hapo awali. Vipi kama tukifanya. . . tukifanya *hivi*? Hatujali, Mungu yuko pamoja nasi.” Walidhani walikuwa sawa, lakini wakakuta kwamba vita vilienda vinginevyo.

Sasa, tunapopanda kwenda kuiteka nchi, tunaona tuko katika hali ile ile. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁵ Mwajua, Akani aliwazia jambo lile lile, alikuwa na amri za Mungu asichukue chochote kutoka kwenye mji huo uliolaaniwa. Nina kama dakika kumi na mbili zaidi. Sina budi kufika kwenye hoteli hiyo. Ninataka kushindilia hili zaidi kidogo, mnaona. Angalieni hapa, hivyo ndivyo tulivyofanya hasa. Mnaona? Vazi zuri la Babeli ambalo Akani alilichukua, na kabari. Alifikiri. . . Huo mji ulikuwa umelaaniwa, na kila kitu ndani yake kililaaniwa; pia imethibitika madhehebu yamelaaniwa. Hilo linasikika la kuchukiza sana, bali ni kweli.

¹⁶⁶ Nilisema muda mfupi uliopita kuhusu mama yangu, angetufanyia, kila Jumamosi usiku, kutokana na kula chakula hicho duni, angetufanya tunywe kipimo kikubwa cha mafuta ya mbarika. Kila. . . Siwezi kuvumilia harufu ya kitu hicho, mnaweza kuyaleta humu chumbani, nami nitashikwa na kiungulia, Kamwe siwezi kuyavumilia, mengi sana. Nami ningechukua na kushikilia pua yangu, ningepanda juu, na ningesema, “Mama, kamwe siwezi kunywa kitu hicho, kinanisonga roho.”

Akasema, “Kisipokusonga roho, na kukuchefua kabisa, hakikufai kitu.”

¹⁶⁷ Hivyo ndivyo ilivyo na kuhubiriwa kwa Neno, kama halikusongi roho, kukuchochea, uanze kusoma (Utoke kwenye maskini hizo kanuni za imani, uje kwenye Neno, uchungeuze uone kama ni sahihi. Kweli.), halikufai kitu. Litachochea maakuli yako ya kiroho. Naam, bwana, linakufanya uanze vizuri.

¹⁶⁸ Hiyo ni njia ngumu, ya kishenzi ya kuelezea, bali ndiyo njia pekee niliyo nayo. Mimi mwenyewe ni mshenzi, wala sina elimu, nina ninii tu, loo, kama Yohana, kitu pekee alichojua kilikuwa ni nyoka, na mashoka, na mambo ya nyikani, na kitu pekee nijuacho ni kile tu nijuacho, na hicho tu ndicho nijuacho, kwa hiyo i—inanibidi tu kulisema jinsi ninavyoliona, na jinsi—jinsi linavyonijia. Lingeweza kuelezewa kwa udhahiri zaidi na vizuri kuliko hivyo, lakini mnajua ninalozungumzia, hilo ni jambo moja, mnaona. Mnajua ninalomaanisha, kwa hiyo jambo ndilo

hilo. Hamna budi kurudi kwenye Neno, mwondokee maskini upuuzi huu wote, kwa vyovyote vile.

¹⁶⁹ Vema. Sasa, Akani aliwazia, “Hilo litakuwa sawa, Nitachukua kabari hii ndogo nzuri, na itakuwa ni maskini vazi zuri. Nami nitakuwa na maskini kitu hiki kizuri *hapa*, nami nitakuwa mzee wa jimbo, na kadhalika, nami ni—nitaninii. . . itakuwa sawa.” Lakini kilikuwa kimelaaniwa! Kila kitu katika mahali hapo palipoanguka kilikuwa kimelaaniwa. Na ndivyo ilivyo siku hizi. Hatuwataki akina Akani, hatutaki ninii. . . Hawangeweza kamwe kupiga hatua na kushinda vita, mpaka kitu hicho kilipoangamizwa. Sawa. Naam, bwana.

¹⁷⁰ Wamisri walidhani ya kwamba ingekuwa ni sawa, Israeli walipitia Bahari ya Chumvi, kwa nini wasingeweza? Wasiotahiriwa, hawakuwa na baraka za agano. Walidhani ilikuwa ni sawa, lakini wakaona kwamba walizama. Huwezi kupitia haya, huwezi kuingia katika ushirika pamoja na Mungu, ukileta mafundisho yaliyobuniwa ulimwenguni. Ulizama, utaangamia pamoja nayo. Huna budi kupitia njia ya Mungu la sivyo hakuna njia. Huna budi kujiweka sawa na Neno, la sivyo uko nje, unafia pale.

¹⁷¹ Kwa hiyo, lakini Misri iliwazia, “Vema, walipitia humo, mimi ninaninii tu. . . sisi ni watu bora kuliko wao, tuna afya zaidi, tuna nguvu zaidi, werevu zaidi. Vema, hao jamaa hata hawawezi kuandika jina lao, nasi ni mabingwa.” Lakini hao mabingwa hawakwenda mbali sana. Mungu haheسابu umahiri jinsi watu wanavyofanya. Hiyo ni kweli.

¹⁷² Wakati wa Nuhu, waliwazia, “Sasa, kama kweli ninii ikija, mbona, sasa, kama kweli ikija mvua kubwa, hapajakuwapo na moja, lakini kama ikinyesha, mbona, tunazo meli na mashua.”

Unasema, “Hawakuwa nazo.” Walikuwa nazo.

¹⁷³ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. . .” namna ile ile. Wanaichimbua miji na kadhalika sasa, iliyozama, iliyo na mifumo yote ya kisasa ya ugavi wa maji, papa hapa Meksiko, miaka michache iliyopita, kila kitu. Hakika. Hakuna jambo jipya chini ya jua.

¹⁷⁴ “Tutaendesha tu meli zetu wenyewe.” Walidhani wangekuwa sawa, lakini Mungu alikuwa na meli moja iliyokuwa itaelea, na hizo zingine zizame. Lakini walidhani ya kwamba meli yao ingedumu, ielele kwa njia yoyote ambayo kitu hiki kingeelea, haidhuru kama kiliundwa Kimaandiko au la.

¹⁷⁵ *Brrrrr!* Ningeweza kusema jambo fulani hapa. Sikilizeni, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Mnafikiri kwamba kitu hicho kitaelea, kitakuwa sawa, kama ni cha Kimaandiko ama sivyo. Hakina budi kuwa cha Kimaandiko kabisa.

¹⁷⁶ Mungu alimwambia Nuhu atengeneze safina hiyo kwa mti wa mshita, na mbao hizo ni nyepesi kuliko za balsa. Hakuna kitu

ndani yake, ni sifongo kubwa mno tu, tupu. Mbona, ningeweza kubeba kizingiti chake kutoka *hapa* hadi *pale*, na, mwisho wa ma- . . . ule ukuta *kule* nyuma, na kingekuwa na unene wa futi sita, ningeweza kukilaza mabegani mwangu na kuondoka nacho. Mbona, si kitu ila sifongo tu, hamna kitu ndani yake, mbao za mshita.

177 Alifanya nini baada ya jambo hilo? Hiyo ilikuwakilisha wewe. Huna budi kuondoa kila kitu kwako, kanuni zako zote za imani na mafundisho yako. Basi Yeye alifanya nini? Alisema, “Itie lami, ndani na nje.” Walipataje lami? Walikata mti na kuutwanga, wakatoa uhai ndani yake, wakatoa lami ndani yake. Kisha wakachukua hiyo lami yenye joto na kuimwaga mle ndani, ndipo sehemu zote tupu zikalowa lami, basi ni ngumu zaidi kuliko feleji yoyote iliyopo. Usingeweza kuukunja, hiyo ndiyo sababu ulistahimili zile hukumu.

178 Kulikuwa na Mtu aliyepaswa kupigwa sana, yule Mwenye haki, Kristo. Tunajifanya tupu, na kumwacha Roho Mtakatifu aingie, Neno la Mungu liingie, hilo linakuimarisha. Hukumu, “Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu.” Mnaona? Haina budi kuwa, loo, naam. Lakini walidhani ilikuwa ni vivyo hivyo tu, mnaona, ilikuwa ni sawa, walidhani ingekuwa sawa.

179 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, wanasema, “Madhehebu yetu, nadhani hilo ni sawa. Loo, usiniambie. Mimi ni . . . Ati Siku za miujiza? Hakuna kitu kama hiki. Sasa, itakuwa sawa, hivi sisi si ni kanisa?” Endelea, ingia tu moja kwa moja hukumuni, hilo ni sawa.

180 Kuna madhehebu mengi sana mbalimbali, hata inasababisha kuchanganyikiwa. Watu, wakidhanzia tu kwamba ni sawa, endeleeni mbele moja kwa moja. Hatujui ni wapi . . . Ni lipi lililo sahihi basi, ni lipi lililo sahihi? Wape jaribio la Neno. Hilo Ndilo linalosema kama ni kweli ama si kweli.

181 Hebu tuone, Kumbukumbu la Torati 22:18, mwajua, ilisema, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana, nitasema naye. Ndipo kama anaambatana na Maandiko, yale asemayo yatatimia tu, itakuwa sawa.” Mnaona? Marko 16 ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yohana 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Haya basi, sasa tunakuwa sawa.

182 Wakati Yohana alipokuja kutambulisha, ni njia gani iliyokuwa sahihi, Mafarisayo walikuwa na njia yao, Masadukayo walikuwa na njia yao, watoza ushuru walikuwa na njia yao, makundi mbalimbali yalikuwa na njia yao, madhehebu yao, mashirika, Yohana hakwenda kwa yoyote ya shule zao, alienda nyikani na kungojea, alilisoma Neno. Muda si muda mwajua, Mungu akamwambia, huko nje nyikani, ya kwamba Masihi huyu

atakuwa na ishara itakayomfuata, kama alivyofanya sikuzote; yale tuliyozungumzia jana usiku.

¹⁸³ Kwa hiyo Yohana akangojea, hakujiunga na yoyote yao, alingojea tu, mpaka alipokuwa na hakika, hakudhania chochote. Akasema, “Sasa, ngoja kidogo, hao *hapo* Mafarisayo, hao ni watu wazuri, ni watu wa utakatifu. Mbona, hakika, wako sawa,” mimi. . . hakufanya hivyo, “Nadhani wako sawa.” Hawakuwa sawa. Mungu. . . Yohana aliingojea ile ishara, Yohana alingojea mpaka alipokuwa na hakika. Mnaona? Bila shaka, alingojea. Hakudhania, alingojea mpaka alipoona ishara ya kweli ya Masihi.

¹⁸⁴ Nathani, alikuwa mwepesi wa kuudhika tu alivyoweza kuwa, akasema tu, “Sasa, siamini jambo hilo, itanibidi kuliona.” Alipofika kule juu na kuona ya kwamba alikuwa ndiye Masihi, aliridhika basi. Hakudhania, alingojea tu mpaka alipoliona.

¹⁸⁵ Malkia wa Sheba, alingojea mpaka akaliona. Akasema, “Sasa, ni za- . . .” Alikuwa ni kafiri, mwajua. Kasema, “Kama nikipanda kwenda kule, mambo haya yote, nitafanya nini?” na kadhalika. “Ninasikia ya kwamba—ya kwamba kuna ninii. . . ya kwamba Mungu wao anaishi ndani ya mtu anayeitwa Sulemani, mfalme wao. Wamempenda sana wakamfanya mfalme. Nami. . . Kama—kama. . . Yeye ni Mungu. . . kama. . . Ni—ninasoma Maneno haya, ikiwa—ikiwa ishara hiyo iko ndani ya mtu huyo, basi mtu huyo ananena habari za Mungu. Nitapanda niende nikaone.”

¹⁸⁶ Kwa hiyo akawatandika ngamia wake, akaanza kuvuka jangwa, ndipo akafika kule juu, akapiga hema lake huko nje, na kungojea, mwajua, naye akangojea. Basi siku ya kwanza, labda, aliketi huko nyuma kabisa kanisani, naye akamwona Mchungaji Sulemani akitokea he—hekaluni, huku watu wake wote wamemzunguka. Na, loo, walikuwa na jambo kuu pale. Sasa, alitaka kuwa na hakika kwamba alikuwa sahihi.

¹⁸⁷ Kwa hiyo basi, muda si muda mwajua, aliona kwamba upambanuzi huo ulikuwa mkamilifu kabisa. Hatimaye, kadi yake ya maombi ikaitwa, naye akapanda jukwaani. Nayu Biblia ilisema hakuna kitu ambacho Sulemani hakujua kumhusu. Hiyo ni kweli. Hakudhania tena.

¹⁸⁸ Akasema, “Yote ambayo nimesikia ni kweli, na zaidi. Ni makubwa kuliko hata niliyoambiwa.” Akasema, “Heri watu walio hapa pamoja nawe, na wanaweza kuona mambo haya yakitendeka siku baada ya siku. Hebu nichukue tu nafasi kidogo hapa, nyuma hapa chini, ili niweze kupiga magoti hapo nitakaporudi. Mungu wenu na awe Mungu wangu.” Hakuwa akidhania chochote, aliangalia na kungojea mpaka alipoona ishara ya kweli ya Mungu.

¹⁸⁹ Yule mwanamke kisimani, alijua Masihi alikuwa yuaja, alijua kile Yeye angefanya. Kwa hiyo haidhuru walifanya

nini . . . Yeye hakudhania, bali mara alipoona hilo, aliangalia, naye akasema, “Ngoja kidogo, hapana shaka Wewe ni nabii.” Alionekana kama, mtu wa kawaida tu. Kasema, “Tunajua kuna Mtu anayekuja, Masihi atafanya *kadhaa na kadhaa*.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

¹⁹⁰ Ndipo huyo akapitia mjini, bila kudhania lolote, “Tokeni, ninyi jamaa, na mlete ninii yenu, mafundisho yenu yote, na mlete vitabu vyenu vyote vya kanuni za imani, na kadhalika, na hebu tuone kama huyu ndiye Masihi. Hebu . . . Hu—huenda ikawa.” Hakudhania lolote, alisema, “Njoni, mwone Mtu niliyemwona!” Amina. Sawa. “Njoo, muone, tulimwona.” Hakukuwa na kosa kulihusu. Hakuwa akidhania lolote, alijua alichokuwa akizungumzia, alijua alikuwa sahihi.

¹⁹¹ Wale wanafunzi, wale wanafunzi huko Pentekoste, vipi kama wanalisema, “Sasa, ngojeni, hebu tuone, ni ninii . . . hebu tuone, Yesu alitupa amri, kwa hiyo Yeye alitwambia tuje huku. Tunajua Bwana wetu hawezi kusema uongo.” Angalieni jinsi dhambi isivyo na hatia, jinsi inavyonyemelea. “Sasa, Yeye alitwambia tungempokea Roho Mtakatifu tutakapokuja juu hapa. ‘Nitaninii . . .’” Sikiliza hili, Daktari. “Loo, mnajua . . . Andrew, njoo hapa kwa dakika moja.”

“Naam, naam, bwana.”

“Mathayo, waonaje?”

“Yohana, njoo hapa. Sasa, unajua Bwana wetu hawezi kusema uongo.”

“Kweli.”

¹⁹² “Yeye alitwambia tungoje hapa mpaka tutakapokuwa, tayari, tumeipokea Ahadi ya Baba, nasi tulikuwa tumpokee Roho Mtakatifu. Nawe unakumbuka, Yeye aliinua mikono Yake juu yetu, na kutupulizia, na kusema, ‘Mpokeeni Roho Mtakatifu?’”

“Naam. Um-hum.”

¹⁹³ “Vema, nawaambieni, Ndugu, naamini *tumempokea*, nadhani tumempokea.” Loo, ewe mnafiki mwenye mashaka! “Ninaamini tumempokea, nafikiri tunapaswa kumkubali kwa imani.”

¹⁹⁴ Enyi Wabaptisti! “Tunampokea kwa imani.” Kwa imani, si kitu! Ni tukio.

¹⁹⁵ Ninaweza kumwona Petro, yule mtu aliyefunzwa, akisimama pale, aliishi pamoja na Yesu, akasema, “Ngoja kidogo, hilo si la Kimaandiko.”

“Vema, nadhani tunaye.”

“Upuuzi.”

“Tunapaswa kuanza huduma yetu. Vema, tayari tumekuwa hapa siku tisa, kwani tunangojea nini?”

“Yeye alisema, ‘Hata,’ sivyo? ‘Hata.’ Si siku tisa, siku kumi, ama hamsini, ama mia moja, Yeye alisema, ‘Ngojeni hata.’”

¹⁹⁶ Hapo ndipo tulipofanyia kosa letu, naam, bwana, tukidhania ni sawa. Wengi wetu tunadhani kwa sababu tulipata kuna kwa lugha ya kwamba hayo ndiyo yote tuliyopaswa kufanya. Hiyo ni kweli. Tulikaa pale na kunena kwa lugha, na mtu fulani akatutia moyo, nasi tukanena kwa lugha, tulidhani hilo lilikuwa sawa, kisha tukarudi nyuma moja kwa moja.

¹⁹⁷ Hiyo ndiyo sababu ninyi wanawake mngali mnakata nywele zenu, mnajipodoa, kaptura, hiyo ndiyo sababu ninyi wanaume mngali mna mambo yenu, na mnaendelea jinsi mnavyofanya, mnadhania tu. Hiyo ni kweli. Komeni! Komeni! Rudini kwenye Neno, kumbukeni.

¹⁹⁸ Ninaweza kumwona Simoni akisimama, akisema, “Ngoja kidogo, Isaya alisema, ‘Amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo.’” Loo, jamani, ninaweza kumwona akirejea kwenye Maandiko. “Hatutadhania lolote, tutangojea hapa mpaka jambo fulani litukie.” Na hiyo ni kweli.

¹⁹⁹ “Vema, nawaambia, Ndugu, acheni waende wakafanye watakalo, tutaunda tu kundi letu dogo, nasi tutajiita *Fulani-na-fulani*. Na tuwaache wakae kama wanataka kuwa walokole.” Haya basi. Hiyo ni kweli.

²⁰⁰ Dumuni na Neno. Paulo alisema, “Walitoka kwetu, kwa sababu hawakuwa wa kwetu.” Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

²⁰¹ Loo, ni wangapi ningeweza tu... Nina Maandiko mengi sana yaliyoandikwa hapa, ingenichukua siku nzima, wala siwezi kukaa zaidi.

²⁰² Wakidhania tu, wakidhania, hivyo tu ndivyo wanavyofanya, wakidhania itakuwa sawa, wakidhani ya kwamba ni sawa.

²⁰³ Danieli, walidhania pale, huko chini katika... walidhani ingekuwa sawa, kuchukua vyombo vitakatifu vya Mungu, na kuvinywea, walidhani ilikuwa ni sawa kuwacheka watu waliokuwa na Roho Mtakatifu, na ilikuwa ni sawa ku—kuwadhihaki. Biblia ilisema, “Ni afadhali ufungiwe jiwe la kusagia shingoni mwako, ukatoswe katika kilindi cha bahari, kuliko hata kumkosesha mmojawapo wa hawa wadogo Wangu.”

²⁰⁴ Ndugu, ninawaona watu hawa wakitembea mitaani, shingo hizi zilizoniyoshwa, za kutamanisha, wamevaa visigino virefu *hivi*, wanawake wamesukumwa mbele, na huko nyuma, na huku na huku namna *hii*. Basi mwanamke fulani aliniambia, kasema, “Mimi. . .” mwanamke Mpentekoste, kasema, “Vema,” amevaa maskini sketi hizi ndogo, mwajua, karibu nusu ya goti lao, kasema, “mbona, Ndugu Branham,” kasema, “hiyo ndiyo aina pekee wanayoshona.” Wanatengeneza cherehani na kuuza vitambaa. Unaona, maskini roho hiyo chafu iko ndani yako.

205 Kwa nini mwanamke Mpentekoste atake kutenda hivyo? Mimi. . . Yeye si Mpentekoste, ana jina tu la Pentekoste. Afadhali niondokee hilo upesi sana, nifungue ukurasa mwingine.

206 Loo, Musa, vipi kama angalidhanja? Uh-huh. Usidhanie, dumu na Neno. Usikubali kitu chochote tofauti, kaa na kile Mungu alisema ukae nacho, dumu na Neno. Amina.

207 Mungu anawajibika, Mungu anawajibika kwa Neno Lake, na kama Neno liko ndani yako, Yeye anawajibika kwako pamoja na Neno Lake. Lakini unapofanya kama Hawa, kutilia shaka chembe moja ndogo Yake na kuingiza kitu fulani ndani badala yake, uko nje, papo hapo. Dumuni na Neno. Hebu tusidhanie chochote, hebu tuchukue tu Kile Neno lisemacho na kuliadini. Mtafanya hivyo?

Sasa, angalieni, enyi marafiki, hilo ni kali, sivyo?

Sina budi kuwa mahali pale katika yapata dakika tano, ama kumi, si—sina budi kwenda, kwa hiyo mimi—mimi—mimi, kwa kawaida, mazungumzo yangu huwa marefu zaidi, lakini si—sina budi kusonga mbele.

208 Lakini, Mungu awabariki. Ni—ninawapenda, simaanishi kuwa katili, simaanishi kuwakatakata na kuwararua, mara nyingi linanikata vibaya sana kuliko linavyowakata ninyi, lakini, Ndugu, Dada, sina budi kukutana nanyi kule, siku moja. Na kama nikisimama pale, Naye akaniangalia, na kusema, “Ewe mdanganyifu! Damu yao inatakiwa mikononi mwako,” mnaona, maana ninajua tofauti, na ole wangu nisipolisema!

209 Sasa, mnaweza. . . Na—naomba tu ya kwamba hamtakosana nami, bali mtachukua tu Neno na kuketi chini mwone kama hiyo si kweli. Yachunguzeni mashirika haya, madhehebu, rudini, u—unawajibika kwa nafsi yako. Mbona, kama kulikuwa na kitu ambacho kingekudhuru kimwili, ungefanya kila kitu ulimwenguni, utatafuta mawakili, wanasheria, na kadhalika kujilinda, uchukue mlinzi binafsi kama maisha yako yalitishiwa, chochote kile, ungefanya hivyo. Unaona? Vipi kuhusu nafsi yako? Uzima Wako wa Milele umeathiriwa.

210 Unapaswa kurudi nyuma na kuona kile kilichoyapata madhehebu, kile daima kimeyapata. Mimi siyapingi madhehebu, watu humo ndani, siwapingi Wakatoliki, Sipingi Mbaptisti, Mpresbiteri. Mbona, kama ningeuliza asubuhi ya leo katika kanisa hili hapa. . . Ninamshukuru Bwana kwa kunipa mamilioni ya marafiki kote ulimwenguni, nao ni Wakatoliki, Wabaptisti, Wapresbiteri. Ni kitu gani?

211 Sasa, hao Wafanyabiashara Wakristo nilio nao sasa hivi, nikienda kote ulimwenguni pamoja na hao watu, ni kwa nini? Ninawaambia vile vile tu ninavyowaambia chochote, nami nilisema hilo hivi majuzi katika mkutano. Ndipo mmoja wa hao viongozi akasimama, akasema, “Hiyo ndiyo sababu tuko pamoja

nawe.” Kasema, “Wewe unadumu na Neno, Nalo linatuweka sawa.” Hiyo ni kweli.

²¹² Watu watakupenda endapo utasema ukweli. Ni wangapi wenu enyi wasichana mnaomthamini maskini mama mzuri ambaye hakuachilia fimbo, bali aliwaweka mmenyooka? Mnamthamini? Vipi kuhusu maskini baba huyo mwenye mvi? Yuko hapa nje makaburini leo hii. Je, unampenda? Kwa nini? Alikuwa ni *baba*. Hiyo ni kweli.

²¹³ Lakini yule aliyekuruhusu. . . Nilimwona mvulana mmoja hivi majuzi, aliiba, na kadhalika, na kufanya yasiyofaa, mbona, mama yake alimwunga mkono, akasema, “Kama mama yangu,” alikuwa akienda gereza, “angelinifanya nirudishe vitu hivyo, nisingekuwa nikienda hapa leo hii.” Haya basi. Unaona? Ni hilo. Usiwe mtu asiye na msimamo, Mungu anakutaka utetee yaliyo Kweli. Amina.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

²¹⁴ Baba yetu wa Mbinguni, sijui, huenda tusikutane tena namna hii. Huenda hii ikawa ndiyo asubuhi yetu ya mwisho pamoja, sijui kabisa. Ninakuomba uturehemu, Baba. Jalia watu hawa baraka Zako.

²¹⁵ Na, Bwana, najua wakati mwingine linakata, na, bali ni Upanga, ni ninii mkali. . . ninii. . . Biblia yako, katika Kitabu cha Waebrania, kilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili.” Nao Upanga huu unaweza tu kushikwa na mkono wa imani, yaani kwa wito dhahiri, Roho wa Mungu nyuma Yake kuliunga mkono na kuonyesha ya kwamba ni Mungu, pamoja na Roho anayeweza kulifanya lithibitisha kwamba ni kweli. Lakini Mungu, jalia watu waione.

²¹⁶ Maskini mtu huyu ndugu yangu mnyenyekevu hapa, Ndugu na Dada Littlefield, hao wawili ni mmoja, na upendo wake na hisani yake, ninakumbuka wakati mmoja walipokuita kwa mtu fulani, yeye alikuwa ni Mrumi, lakini wakasema, “Amelifanyia taifa letu mambo makuu, ametujengea sinagogi, anastahili.”

²¹⁷ Basi, Mungu, nikiketi chini ya upako kando ya huyu mtu, ninajua ndani ya moyo wake ananipenda, analiamini, analijua. Nami nampenda, Wewe unajua hilo, Bwana. Nami nimemwambia saa zisingeweza kuwa ndefu sana, wala usiku kuwa giza kupita kiasi, ama mvua kunyesha kwa nguvu kupita kiasi, ila wakati wowote ambapo ningeweza kuunganisha mioyo pamoja naye kuliombea maskini kusanyiko lake, kufanya lolote niwezalo, mradi tu haikuwa kinyume na uongozi Wako, ningefanya hivyo. Anajisikia vivyo hivyo kwangu mimi.

²¹⁸ Sasa, Bwana, jalia baraka zangu zikae juu yake. Tujalie, Bwana. Na maskini kanisa lake dogo hapa, nikisimama hapa ukumbini pamoja na hao wavulana muda mfupi uliopita, na kumsikia akisimulia kuhusu, wakati mtu fulani aliposema, “Utawafanyia nini maskini?” Akasema, “Nitawachukua niende

pamoja nao.” Hiyo ni kweli, Bwana, huyo ni Roho wa Kristo ndani yake, kama vile Musa alivyojitupa kwenye pengo na kusema, “Bwana, nichukue mimi, waache,” Roho wa Kristo ndani yake.

²¹⁹ Ninaomba ya kwamba Wewe umsaidie Ndugu Littlefield na Dada Littlefield. Wape, Bwana, u—uweza wa Roho wa Mungu. Jalia wabarikiwe. Jalia ninii yao . . . Jalia wawalishe watu hawa, Bwana, kimwili na kiroho. Tujalie, Bwana.

²²⁰ Libariki maskini kanisa hili, wabariki mashemasi, wadhamini. Jalia maskini kanisa hili lisimame, na kutoka mahali hapa padogo hapa, wakati Unyakuo utakapokuja, jalia kuwe na angalau dazani kadhaa watakaoondoka hapa katika Unyakuo. Waone hawa wazee, wanyonge, hawa wanawake wakongwe, wenye mvi, makunyanzi usoni, wamwone yeye na baba wakiwa na watoto wao karibu nao, wajukuu wao wamesimama, wote mara moja, wamwone babu akigeuka kuwa kijana mwanamume, nyanya, akiondoka basi.

Loo, vazi hili la mwili tutaliangusha, na
kufufuka

Tunyakue thawabu ya milele,
Tupaze sauti, huku tukipitia hewani,
“Kwaheri, kwaheri!”

Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawabariki.

²²¹ Na kama nimefanya jambo lolote baya, kama nimemkata ama kumwudhi mtu yeyote, Bwana, Si—sikumaanisha kufanya hivyo kwa njia hiyo, labda kulikuwa na kitu kilichohitaji kukatwa, kwa hiyo ninaliweka tu Neno pale, Hilo ni Mbegu, sasa, hebu litokee kama Zao kuu. Jalia atokee Roho kama huyo katika kanisa hili, Bwana, kwamba nguvu za Mungu zitajulikana katika maeneo yote ya karibu. Jalia kutoka hapa watoke wamishenari, kutoka hapa watoke wachungaji maarufu. Tujalie, Bwana. Wape hao Chakula, Chakula cha Kondoo Bwana, wanatamani Chakula cha Kondoo, Neno Lako.

Jitukuze Mwenyewe, Baba, katikati yetu, kwa Jina la Yesu.

Sasa, Bwana, wakiwapo wale hapa, leo, wasiokujua Wewe, jalia wakukubali sasa, katika Jina la Bwana Yesu.

²²² Huku tumeinamisha vichwa vyetu, ninataka swali aminifu kabisa lijibiwe: Je, unajisikia ya kwamba unatembea katika Nuru ya Mungu? Sitakuuliza ikiwa hujisikii, bila shaka u—unadhania tu sasa, lakini ndani ya moyo wako, unajua ya kwamba kuna mambo yaliyoandikwa katika Biblia hiyo upate kuyafanya, nawe huyafanyi, na mradi tu mnafanya hivyo, eni marafiki, msidhanie, hebu tuwe sawa.

²²³ Hutahukumiwa kwa kanuni zako za imani, hutahukumiwa kwa hisia zako, utahukumiwa kwa Neno hili. Na kama unajua umekuwa makosani, huku kila kichwa kimeinamishwa na

jicho limefumbwa, hivi mtainua tu mikono yenu, na kusema, “Niombe, Ndugu Branham. Ninaomba sasa kwamba Mungu atanisaidia?”

Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe, wewe. Mungu awabariki. Hilo ni sawa. Kuwa mwaminifu. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki.

Mungu asifiwe. Ninakuona. Nimemwona mwanamke akiponywa, papo hapo, mgonjwa, ameketi papa *hapa*, maana aliinua mkono wake, alikuwa mwaminifu, akaponywa.

Mungu akubariki, bwana. Sawa.

²²⁴ Unasema, “Ndugu Branham, unajua je jambo hilo?” Najua hilo. Naam, bwana, Mungu awe pamoja nawe. Kuwa tu mwaminifu. “Ninajua sininii. . .” Mungu akubariki, wewe, wewe. Naam. Madazani yao. Mungu awabariki.

²²⁵ Yeye anaona. . . Yeye. . . Huenda nikaukosa mkono wako, bali Yeye haukosi, Yeye hana kikomo. Alijua kila kiroboti ambaye angekuwepo duniani kabla ya dunia kuumbwa, ni mara ngapi angeyapepesa macho yake, na angepata shahamu kiasi gani. Hakika, ni Neno la Mungu lililonenwa, kila sehemu yake. Anajua. . . Yeye hana kikomo. Alijua kile. . . Asiye na kikomo, neno linakuja *bila kikomo*, mnaona. Unaninii tu. . . Yeye hana kikomo. Halielezeki, huwezi kulielezea. Ni la Milele. Yeye ni wa Milele, anajua kila kitu, hata wazo. Kila wazo ungepata kuwazia, Yeye alilijua kabla hujazaliwa. Hiyo ndiyo sababu kwa kutangulia kujua Yeye angeweza kuchagua tangu zamani, Yeye anajua utakalofanya, Yeye anaweza kuyafanya yote yatende kazi kwa utukufu Wake.

²²⁶ Mbarikiwe. Nimekuja kwenu katika Jina la Bwana. Wakati mmeinamisha vichwa vyenu, nimejaribu, nimehubiri kwa nguvu sana, lakini ni—ni kweli. Sasa, jana usiku tulikuwa na ibada ya uponyaji, bali ninajisikia kuongozwa kufanya jambo fulani sasa hivi. Ninaona, bado, watu hapa ambao ni wagonjwa, wahitaji. Acha Mungu anene kama nimewaambia kweli au la. Acha Mungu aseme nawe.

²²⁷ Baba wa Mbinguni, sasa nena, nimenena, sasa Wewe nena, ukithibitisha kwamba ni kweli. Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu.

²²⁸ Sasa, ninataka, kila mtu humu ndani aliye mgonjwa, ninataka angalau, nipate wawili au watatu kwa ajili ya ushuhuda kabla sijaondoka hapa, na kumrudishia ibada Ndugu Littlefield. Sasa, iweni tu katika maombi. Sasa, wewe omba, na kusema, “Bwana Yesu, inasema katika Biblia ya kwamba tunaye Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

²²⁹ Sasa, kama huyo Kuhani Mkuu ni Yesu Kristo, wote wanaoamini hilo semeni, “Amina.” Mnaamini Yesu ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Yehova? Mnaamini Yeye yu hai? Na hivi sasa

Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, yu hai milele apate kutuombea tunapoungama? Na kama Yeye ni Kuhani Mkuu aliye hai, alifanyaje? Wakati alipokuwa Kuhani Mkuu hapa duniani, mwanamke mmoja siku moja aligusa vazi Lake, naye akageuka na kumwambia ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Je, hilo lilikuwa tendo la Kuhani Mkuu? Basi Yeye ni Kuhani Mkuu wa Milele; basi Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

²³⁰ Sasa, Yeye ni Mzabibu, hebu nijitwae tu mwenyewe, kama mngenisamehe, na Mungu anirehemu, Nitakuwa tawi, hebu lizae matunda Yake, tuone kama tuko kwenye wakati wa mwisho ama hatuko. Ombeni.

²³¹ Kama Hilo...Ninaliona likimfunika ki—kijana mwanamume, bali ninamjua huyo mtu. Ninaiona Nuru hiyo ikining'inia moja kwa moja juu ya mvulana fulani, akiniangalia moja kwa moja, bali ninamjua. Yeye ameponywa (sitaninii...) hapo kabla. Atakuwa mzima sasa, bali sitasema neno juu yake.

²³² Hii papa hapa karibu nami, yapata safu ya pili au ya tatu nyuma. Iko juu ya mwanamke aliye na matatizo. Simjui. Natumaini atalipata. Bwana, niambie yeye ni nani. Binti Cox, amini. Unaamini? Unaweza kupokea kile unachoomba.

²³³ Mwanamke aliyeketi karibu, karibu sana, ana vipindi vya kusongwa roho. Hatufahamiani, sikujui. Bibi Allaway, hiyo ni kweli. Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Unaamini? Amina. Amini, usiwe na shaka.

Sasa, unaamini? Nini kilitukia? Alimgusa Kuhani Mkuu. Mnaweza kuelewa?

Vipi kuhusu wewe unayeketi hapo, mama unayeomba, una shida ya kinyumbani? Bibi Miller, mume alifanya makosa, akatoroka na mwanamke huyo.

²³⁴ Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, Mungu Mbinguni anajua hilo ni kweli. Alifanya nini? Kamwe hakunigusa, yuko futi thelathini kutoka kwangu, bali alimgusa Kuhani Mkuu.

²³⁵ Ni kitu gani? Injili hii ninayowahubiria ni kweli. Mnaamini hilo? Basi tembeeni katika Nuru. Tembea katika Nuru ya Injili. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote. Je, utamkubali? Je, uta—utaondoka kwenye kanuni zote za imani na chochote kile, na kumkubali Masihi, Roho Mtakatifu wa Kristo? Unaamini kwa moyo wako wote? Inueni mikono yenu. Sasa, ni kitu gani hapa?

Hao walikuwa wangapi? Hao walikuwa wawili? Wangapi? Watatu? Watatu. Hao wanatosha. Hao wanatosha. Ninaiona juu ya mwanamume fulani, imening'inia papa *hapa* pembeni. Mnaona?

²³⁶ Ninawaambia nini? Huyo si mimi ninayewaambia, Huyo ni Mungu akiwaambia sasa. Mwanadamu anaweza kusema

lolote. Tuna mambo mengi sana kote ya bandia yanayoitwa upambanuzi, “Bwana ananiambia mtu fulani humu ndani ana ugonjwa wa figo. Ni nani? Wametoka wapi? Vipi kuhusu wao?” Ni uigaji, kudhania. Hivi hamtambui yale Maandiko yasemayo kuhusu siku hii ya mwisho? Hivi hamtambui jambo la mwisho tunalopaswa kupokea? Ilisema nini katika Malaki 4, kabla tu ya vivuli vya jioni kushuka?

²³⁷ “Loo,” unasema, “hilo lilitimizwa katika Yohana.” Halikutimizwa, Malaki 3 ilitimizwa wakati Yohana alipokuja. Malaki 4, Yeye alisema, “Kabla tu ya ile siku ambayo Bwana ataihukumu dunia na kuiteketeza kwa Moto...” Basi kama Mungu hakuiteketeza dunia kwa Moto wakati Yohana alipokuja, basi si wakati huo, yeye alikuwa ni Malaki 3. Malaki 4 itatimia hivi karibuni sasa. Sasa ndipo inapopaswa kuwa.

²³⁸ Sasa, hatudhanii lolote, tunaliona, tunajua ya kwamba Mungu yuko hapa, Roho Mtakatifu, yule Mkuu, Mungu wa Eliya, Roho Mtakatifu, Shahidi wa siku za mwisho, akiivuta huduma Yake moja kwa moja Kanisani, jambo lile lile ambalo Bwana wetu alifanya.

²³⁹ Kuhani Mkuu anashuka kutoka kwenye Kiti cha Enzi kuingia Kanisani. Nalo Kanisa linajilundika kwa Neno, maana Yeye anaweza tu kuja kwenye Neno, Yeye ni Neno. Neno haliwezi kuja kwe—kwenye shajara, halitatoshea, kwa hiyo Neno halina budi kuja kwenye Neno. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu... Mtu ataishi, Neno lote la Mungu.” Hili *hapa*, liaminini, likubalini basi. Sasa, na tuombe.

²⁴⁰ Asante, Bwana. Kama sitarudi kwenye kanisa hili zuri tena, kwenye ile Siku ya Hukumu damu haiko mikononi mwangu, nilikatakata na kurarua, na kufanya kila kitu, Bwana, inaonekana kama yangekuwa, ya kutosha kumwua mtu.

²⁴¹ Kama wakiendelea, na kanda hizi papa hapa, wote kote ulimwenguni, kama wataendelea baada ya kuona jambo hili, na kujua ni kanda ya sumaku... Mambo haya yanatukia, si kubahatisha, si kitu unachodhania, bali kitu ambacho kimefunuliwa kiroho katika Neno, na kuthibitishwa kuwa hivyo, basi miongoni mwetu asubuhi ya leo yupo yule Mpendwa, Roho huyo Mtakatifu atakayesimama pale Siku hiyo na kutukumbusha jambo hili. Kanda kubwa ya sumaku ya Mungu itachezwa Siku hiyo.

²⁴² Mungu, nirehemu sasa, lirehemu Kanisa, lirehemu kusanyiko hili hapa asubuhi ya leo. Warehemu hawa watu maskini, Bwana, wengi wao wanaongozwa kwa njia ya kila namna na manabii wa uongo, wakidanganywa, maajabu ya udanganyifu, yasiyo ya kimaandiko, damu, moto, moshi, Ee Mungu, yasiyo ya kimaandiko, ya udanganyifu. Biblia ilisema ingekuwa hivyo.

²⁴³ Mungu, wanafikiri unajaribu kusukumia kitu fulani huku. Nifanye nini, Mungu? Sijui la kufanya, Mungu. Wanafikiri labda unajaribu kuwa mjua-yote, ama . . . Naomba ya kwamba utanyosha hilo mioyoni mwao, Bwana, uwajalie wajue ya kwamba ni Wewe, ni Roho Mtakatifu akithibitisha Neno Lake kuwa kweli.

²⁴⁴ Kuna mikono mingi sana iliyo inuliwa muda mfupi uliopita, Bwana, washiriki wa kanisa na kila kitu, wakiinua mkono wao, Wewe ukiufunua kila mkono inapoinuliwa, “Huo *hapo* moyo wao, *hivyo* ndivyo ilivyo,” nikiona hali yao, baadhi yake ni dhambi isiyoungamwa. Ee Mungu, uturehemu. Ninaomba ya kwamba kila mmoja, aliyeinua mkono wake hatakutana na Hukumu, huko ng’ambo, ya Mungu. Jalia waiepuke ile Hukumu, na waende katika Unyakuo, kama vile Nuhu alivyopanda juu ya ile Hukumu, tujalie, Bwana, kama Ibrahimu, tuwe nje ya Hukumu. Turehemu, naomba.


Wabariki watu hawa sasa, wasamehe dhambi zao. Jalia utamu, na utulivu, na wema wa Roho Mtakatifu ukae juu ya kila mmoja wao.

²⁴⁵ Wewe ni Mungu, nami ninakupenda, Bwana. Loo, nakuabudu Wewe, Ewe Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni! Loo, laiti ningaliweza kuunyosha mkono wangu na kukukumbatia Wewe, Bwana! Mimi sistahili, jalia niguse mguu Wako ama chochote kile, Baba. Ninajua Wewe umesimama papa hapa, papa hapa jukwaani, yule Mwenye utukufu, mwenye makovu ya misumari, yuko karibu sana, sana, katika ulimwengu mwingine, kiwango kingine, amesimama hapa.

²⁴⁶ Tunaona shinikizo Lako na nguvu za Roho Wako zikitenda kazi miongoni mwa miili yetu, Bwana, loo, watu wazindi jinsi tulivyo, halafu basi, Wewe ukitembea miongoni mwetu, na kututakasa kwa Damu Yako kulitimiza Neno Lako, na kumsukuma Roho Wako Mtakatifu ndani yetu kutujulisha mambo yaliyopita, yajayo, yaliyopo.

²⁴⁷ Ee Mungu, Wewe ni Mungu. Jinsi ninavyokupenda, Bwana, loo, jinsi ninavyokuabudu! Loo, si ajabu hatuwezi kupata Jina kwa ajili Yako: Wa Ajabu, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele; loo, Ninyoro la Bondeni, Ua la Uwandani; Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi; Neno, Uzima, Furaha, Yote.

²⁴⁸ Wewe ni Mungu. Jinsi ninavyokupenda, Bwana! Ninakusifu, ninakuabudu Wewe usiye na kifani, Wewe Mkuu wa Milele, uliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, sasa uko hapa katika Nguzo ya Moto, ukitembea hapa, ukijionyesha Mwenyewe, Nguzo ile ile ya Moto wakati ilipokuwa katika mwili ulioitwa Bwana Yesu, Mwana wa Kwanza, Mwana wa pekee, sasa kupitia wana waliopewa mamlaka, ikionyesha ya kwamba Wewe ungali ni Mungu.

²⁴⁹ Hatujapotea, tumeokolewa. Hatuko katika kule kuanguka, hatuko katika madhehebu, hatuko katika kanuni za imani, tuko katika nguvu na kufufuka kwa Mwokozi wetu. Jinsi tunavyokusifu Wewe, Bwana, kwa ajili ya wema Wako! 

62-0408 Kudhania
Church Of Faith
Cleveland, Tennessee Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org